# KRISTO NA KANISA LA KWANZA
# (MWALIMU)



## VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

**Mwaka wa Kwanza** **Kitabu cha Pili**

# KRISTO NA KANISA LA KWANZA

# (MWALIMU]

**VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA**

**Mwaka wa Kwanza** **Kitabu cha Pili**

Africa Coordinated Curriculum for Bible Study

J1 - 2TS

With permission of International Publications Services

**Published and printed by**
**Baptist Publications House**
**Box 30370, Thika Road, Nairobi**

© Copyright, 1988
Baptist Publications House
All Rights Reserved

Nayaweza mambo yote katika anitiaye nguvu. (Wafilipi 4:13)

## MITUME WATISHWA

Watu wengi waliosikia mahubiri ya kwanza ya Petro walihuzunika juu ya dhambi zao. Lakini Kuhani Mkuu na wengine waliokuwa barazani walikasarika waliposikia ujumbe huu. Walitaka kuwaua Petro na mitume wengine. (Matendo 5:33)

## HABARI ZILIZOTUFIKIA

Mwingine atoka ndani ya Gereza lililo fungwa! (Matendo 12:1-9)

Gereza hili ndimo alimofungwa Petro, kiongozi wa Wakristo ambaye alitolewa humo usiku. Hakuna kitu kilichopatikana ndani ya gereza isipokuwa minyororo ambayo inaonyeshwa katika picha.

## KORNELIO, AKIDA WA KIRUMI, AGEUKA KUWA MKRISTO. (Matendo 10)

KAISARIA - Kwa Mshangao wa kila mmoja, Petro aliwahubiria watu wa taifa katika nyumba ya Kornelio, akida wa jeshi la Kirumi. Mbeleni, Injili ilikuwa ikihubiriwa

Wayahudi tu. Lakini Petro alihubiri kwamba, mtu ye yote akimwamini Yesu Kristo, atapata "Ondoleo la dhambi." (Matendo 10:43) Waamini wote wapya walibatizwa.

## Mkuu Wa Malkia Wa Kushi Amwamini Yesu

GAZA - Malaika wa Bwana alimwambia Filipo aondoke katika mji wa Samaria, aende katika jangwa lililokuwa karibu na Gaza. (Matendo 8:26)

Filipo alikutana na mkuu kutoka Kushi ambaye alikuwa ndani ya gari. Filipo alimhubiria Habari Njema za Yesu.

Mkuu huyo naye aliamini kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu.

Kisha Filipo akambatiza. (8:38)

Mkuu huyu wa Kushi alikwenda zake akifurahi. (8:39)

Mkuu huyo alifurahi sana kwa kuwa Mkristo. Kulingana na habari iliyopatikana baadaye kutoka Kushi, Mkuu huyo anawaambia watu wa nchi yake kwamba Yesu ndiye Mwana wa Mungu, ambaye alikufa kwa ajili ya dhambi zao, kisha akafufuka katika wafu na sasa yu hai.

## Filipo Ahubiri Katika Samaria

SAMARIA: Filipo, Mwinjilisti, alihubiri Kristo kwa watu. Furaha uu iliingia jini kwa sababu wagonjwa wengi na viwete waliponywa. Watu wengi walimwamini Yesu (Matendo 8:5-8). Simoni, mchawi, pia alimwamini Yesu. Lakini alitaka kuwapa Petro na Yohana fedha ikiwa wangalimpatia kipawa cha Roho Mtakatifu. (Matendo 8:9-20)

Petro na Yohana walimkemea mchawi huyu. Simoni aliogopa. Aliwauliza mitume kumwombea ili kwamba asiadhibiwe kwa kutaka kununua uwezo kutoka kwa Mungu.

# GAZETI LA YERUSALEMU

**TOLEO MAALUM**

**MAKUHANI WAWASHIKA MITUME WA YESU WALIOMPONYA MTU ALIYEKUWA KIWETE KWA MIAKA AROBAINI**

Lakini Udhalimu Huongeza Idadi ya Wale Waaminio ya Kuwa Yesu Ndiye Mwana wa Mungu.

Namba zilizoko mkono wa kushoto zaonyesha kuzidi kwa kanisa la Kristo.Jaza nafasi zilizoachwa kwa kuandika namba utakazopata baada ya kusoma maandiko hayo hapo chini.

| Namba ya Washiriki | Maandiko |
|---|---|
| 12 | Mitume wa kwanza (Mathayo 10:2-5) |
| 11 | Baada ya Yuda kumsaliti Yesu. |
| 500 | Majuma machache tu baadaye. (1 Wakorintho 15:6) |
| 3000 | Baada ya mahubiri ya-kwanza ya Petro. (Matendo 2:41) |
| 5000 | Baada ya mahubiri ya pili ya Petro. (Matendo 4:4) |

**HABARI MUHIMU**

**Mitume Watoka ndani ya Gereza Lililofungwa!**

YERUSALEMU -- Mitume wa Yesu ambao walifungwa gerezani jana na Kuhani Mkuu walipatikana leo alfajiri. Mashujaa hawa walikuwa wakihubiri katika hekalu. Wanadai ya kuwa malaika ndiye aliyefungua milango ya gereza. (Matendo 5:17-21)

**MVUVI - MTUME PETRO ADAI KWAMBA,**

"YESU, MNAZARETI, YU HAI!"

Awashtaki wakuu wa Wayahudi kwa kumwua Yesu. Asisitiza kwamba Mungu Amemfufua Yesu kutoka kwa wafu. Mji wote wa Yerusalemu ulikuwa na kelele leo. Wafuasi wanyenyekevu wa Yesu waligeuka kuwa mashujaa. Wanasema kwamba Mungu alimfufua Yesu katika wafu. (Matendo 3:15) Huyu Yesu alisulibiwa juzijuzi (Luka 23:33) baada ya huhukumiwa mbele ya baraza la Wayahudi (Luka 22:66), na pia mbele ya Liwali Pilato. (Luka 23:24) Wayahudi wali-mwamuru Liwali amhukumu Yesu kufa.

Ni jambo lenye kushangaza kwamba katika Siku ya Pentecoste wafuasi wa Yesu ambao hawana elimu waliweza kusema kwa lugha nyingine. (Matendo 2:1,4) Watu wa nchi nyingine ambao walikuja Yerusalemu kuadhimi-sha sikukuu hiyo, waliweza kuelewa kila neno walilosema.



# KRISTO NA KANISA LA KWANZA

**Mwaka wa Kwanza** **Kitabu cha Pili**

## YALIYOMO

**Sura** **Ukurasa**


1. Malme Yesu ........ 5
2. Yesu Alikula na Wanafunzi wake ........ 10
3. Yesu Anahukumiwa na Kusulibiwa ........ 16
4. Yesu Afufuka Katika Wafu ........ 22
5. Mtu Aliyeahidiwa ........ 28
6. Mahubiri Yenye Nguvu ........ 33
7. Petro Na Uwezo wa Mungu ........ 38
8. Mashahidi Wenye Ushujaa ........ 43
9. Mashahidi Gerezani ........ 48
10. Shahidi Aliyekufa Kwa Ajili ya Kristo ........ 54
11. Kazi ya Filipo Jangwani ........ 60
12. Watu Wa Mataifa Wasikia Habari Za Wokovu ........ 66
13. Gazeti La Yerusalemu ........ 71

ushuhuda wao, injili ya Bwana ilienea haraka sana. Katika wakati ule wa wanafunzi kumi na wawili, injili ilienezwa ulimwenguni kote.

Kama kungalikuwapo na magazeti nyakati zile, yangalijaa maajabu ya kazi ya Wakristo. Tunaweza kuwa sehemu ya mambo yale ya ajabu ambayo yalifanyika karibu na Jerusalemu nyakati zile!

## KAZI YA KUFANYA

Kazi ya kufanya ya somo hili ni kama mfano wa gazeti. Wasaidie wanafunzi wako kujaza nafasi zilizoachwa. Bila shaka watahitaji kutumia Biblia ili waweze kupata majibu yaliyo sawa.

## KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

Tazama tena vifungu vya kukumbuka vya masomo yote yaliyopita.

"Wakasema, 'Ndiye mbarikiwa Mfalme ajaye kwa jina la Bwana; amani mbinguni, na utukufu huko juu'" Luka 19:38

"Akatwaa mkate, akashukuru, akaumega, akawapa, akisema, Huu ndio mwili wangu unaotowela kwa ajili yenu." Luka 22:19

"Yesu alijitoa nafsi yake kwa ajili ya dhambi zetu, ili atuokoe na dunia hii mbovu iliyopo sasa." Wagalatia 1:4

"Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko; na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alufufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko." 1 Wakorintho 15:3b, 4.

"Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? 1 Wakorintho 3:16

"Na itakuwa kila atakayeliita jina la Bwana ataokolewa." Matendo 2:21

"Mwimbieni Bwana, nchi yote; tangazeni wokovu wake siku kwa siku." 1 Mambo ya Nyakati 16:23

"Iweni hodari na moyo wa ushujaa, msiogope wala msiwahofu; kwa maana Bwana, Mungu wako, yeye ndiye anayekwenda pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha." Kumbukumbu la Torati 31:6

"Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu." Matendo 5:29

"Lo lote mkono wako utakalolipata kulifanya, ulifanye kwa nguvu zako." Mhubiri 9:10a

"Uniendeshe katika mapito ya maagizo yako, kwa maana nimependezwa nayo." Zaburi 119:35

"Huyo (Yesu) manabii wote humshuhudia, ya kwamba kwa jina lake kila amwaniniye atapata ondoleo la dhambi." Matendo 10:43

## WAKATI WA KUFUNGA

Funga darasa kwa kumwomba Mungu ili sisi sote tuwe na tamaa ya kuwa wajumbe wa Kristo, na kuweza kuonyesha upendo wa Kristo kwa wengine.

# MARUDIO: GAZETI LA YERUSALEMU

**MASOMO YA BIBLIA: Maandiko yote yaliyotumiwa katika masomo ya kitabu hiki.**

**KUJIANDAA KUFUNDISHA**

Siku ya leo, utawongoza wanafunzi wako kurudia mambo yote yaliyotukia katika masomo ya kitabu hiki. Ingekuwa bora kwako kuangalia tena masomo yote yaliyopita ya kitabu hiki ili uweze kuyakumbuka tena. Pia ingekuwa bora kwako kurudia vifungu vyote vya kukumbuka vya masomo haya. Kusudi la somo hili ni kuonyesha kwamba uwezo wa Mungu unaweza kutusaidia kuwa waamini watiifu na wanaosaidia, na kuhusika na wokovu wa wengine.

**MAMBO YA KUKAZA**

Kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, tunaweza kuwa wajumbe wa Kristo, kwa kuonyesha upendo wetu kwake, na kwa kuwapenda wengine.

**KULIFUNDISHA SOMO**

Je! ni siku gani unayofikiria kuwa siku ya huzuni kubwa katika historia ya mwanadamu? Ndiyo, ni siku ile Yesu alipokufa msalabani. Lakini sisi tunaiita "Ijumaa Njema." Siku hii haikuwa njema isipokuwa tu tukiweza kutambua maana yake hasa.

Siku ile Yesu alipokufa msalabani inaitwa "Ijumaa Njema" kwa sababu ya baraka kubwa na wema ambao umepatikana ulimwenguni kwa ajili ya kifo cha Yesu. Alitoa maisha yake msalabani ili kila mtu amwaminiye yeye aweze kuokolewa.

Siku iliyokuwa ya furaha kuu kwa wanafunzi wa Yesu na kwa ulimwengu wote ni siku ile ya ufufuo wake; siku tunayoiita "Pasaka." Ilikuwa siku ya furaha kuu kwa wanafunzi kwa sababu Yesu alikuwa hai tena, akithibitisha kwamba yeye hakuwa nabii mkuu ambaye angeweza kufanya kazi ya ajabu, bali pia alikuwa Mwana wa Mungu. Alikuwa na uwezo wa kushinda mauti.

Sasa Yesu anakaa mbinguni (Marko 16:19); anatuandalia mahali (Yohana 14:2); anatuombea (Warumi 8:34). Siku moja atarudi tena duniani kuwachukua wale ambao wamekwisha kumpokea kuwa Mwokozi wao, na kukaa naye mbinguni (Yohana 14:3 na 1 Wathesalonike 4:16,17).

Kanisa la Yesu Kristo lilikuwa tokeo la wakati mzuri katika historia ya ulimwengu. Warumi walikuwa wamejenga barabara nzuri ambazo wanafunzi wa Yesu walisafiria kwenda kueneza injili katika kila mji, hata wakati walipokuwa wakikimbia kutoka kwa wale waliokuwa wakiwatesa. Wayunani walikuwa wameleta lugha ambayo ilitumiwa na wafanya biashara. Watu wote walielewa lugha hiyo.

Kwa sababu ya Wakristo wa kwanza waliompenda Bwana, na ambao walikuwa waaminifu katika





# MFALME YESU

**MASOMO YA BIBLIA: Luka 19:28-41**

**KUJIANDAA KUFUNDISHA.**

Jiulize mwenyewe swali lile ambalo liko katika kitabu cha wanafunzi. Ungefanya nini kama ungejua kwamba umebaki na juma moja tu kuishi? Je, ungejifunza somo hili? Au ungeendelea kujishughulisha na mambo yako mwenyewe? Inakubidi ufikirie kwamba Yesu alijua kwamba alibaki na juma moja tu kuishi. Wakati unapofundisha somo hili, kumbuka kuwajulisha watoto habari hizi. Wakati wa juma lake la mwisho kuishi, Yesu alikuwa mwaminifu kuifanya kazi ile ambayo Mungu alimpa aifanye. Fikira zake zilikuwa juu ya wengine.

Watu hawakuelewa vizuri mafunzo mengi ya Yesu. Moja, kati ya mafunzo haya ni kuhusu Masihi. Tangu siku ya Musa na Ibrahimu, Wayahudi walikumbuka ahadi ya Mungu ya kuwabariki. Waliamini kwamba siku moja Mungu angemtuma Mwokozi. Walimwita mwokozi huyo aliyeahidiwa "Masihi". Mungu alikuwa amewatunza Wayahudi katika njia maalum. Alikuwa amewapa mana walipokuwa jangwani, na akasaidia majeshi yao kushinda vita. Msaada wa Mungu ulifanya maisha yao hapa duniani kuwa bora. Wayahudi walimfikiria Kristo kuwa atawaletea maisha mazuri hapa duniani. Walifikiri kwamba angeketi katika kiti cha enzi, na kuwa na jeshi ambalo lingeweza kuwashinda maadui zake. Hata wale wafuasi wake ambao waliamini kwamba Yesu alikuwa Masihi, walifikiri kwamba Yesu angeanzisha ufalme wake hapa duniani. Walishindana kwamba ni nani ambaye angekuwa mkuu katika ufalme wa Yesu, na kwamba ni nani angeheshimiwa zaidi.

Yesu alijua vile watu walivyofikiria. Alitumia juma hili lake la mwisho kujaribu kufundisha kwamba ufalme wake ulikuwa wa moyo na roho. Yesu alijua kwamba ni akili ya mwanadamu ambayo hutawala mwili. Alijua kwamba roho ya mwanadamu ni lazima itakaswe ikiwa mwanadamu atakuwa mtakatifu. Kusudi la somo la leo ni kuonyesha kwamba ufalme wa Mungu ni wa Roho.

Omba ili Mungu akusaidie kulielewa vizuri somo hili ambalo ni la maana. Kisha utaweza kuwasaidia wanafunzi wako kulielewa.

**MAMBO YA KUKAZA:**

1. Mungu aliwaaahidi Wayahudi kwamba angemtuma Masihi au Mwokozi.

2. Masihi huyu angeleta utawala wa kiroho na amani.

3. Fikira za Yesu zilikuwa juu ya watu wengine si juu yake mwenyewe. Hata wakati wa kufa

kwake msalabani ulipokaribia hakuacha kuwafikiria wengine.

4. Yesu alikuwa mwaminifu katika kuifanya kazi ambayo Mungu alimpeleka kuifanya hata ingawa angekufa baada ya siku chache.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

Mwulize mmoja wa wanafunzi katika darasa lako amwongoze katika maombi. Maombi hayo yawe ya kumwuliza Mungu ayabariki mafunzo. Yawe yanamwuliza Mungu awasaidie wanafunzi katika kuelewa maana ya somo hili.

Kisha waulize wanafunzi swali hili: "Ungefanya nini kama ungejua ya kwamba umebaki na juma moja tu kuishi?" (Toa nafasi ya mazungumzo.)

Wanafunzi wanapaswa kufungua vitabu au Biblia zao katika somo la leo. Somo hili linapatikana katika Luka 19:28-41.

Yesu alikuwa akisafiri kwenda Yerusalemu. Alitembea katika njia iliyokuwa na mavumbi mengi. Njia ile ilipitia kwenye mlima wa Mizeituni hadi kufika Yerusalemu. Wakati wa sikukuu ya Pasaka ulikuwa uko karibu sana. Ye yote aliyeweza kwenda Yerusalemu alisafiri hadi huko kwa ajili ya Pasaka. Yerusalemu ulikuwa mji mkuu wa zamani wa Mfalme Daudi, na ulikuwa mji mtakatifu wa Wayahudi kwa miaka mingi. Hekalu la Herode lilikuwako huko, na kila mmoja alitaka kula karamu mjini Yerusalemu. Watu wengi walikuwa wakienda huko na kila barabara ilikuwa imejaa watu.

Soma vifungu 28-31 katika Luka 19 uone jambo lililotukia mjini. Uliza swali hili: "Kwa nini Yesu aliwatuma wafuasi wake kwenda kumleta mwana-punda?" (Jibu swali hili wewe mwenyewe.)

Yerusalemu ulikuwa mji wenye historia ndefu na maadui wengi. Mara kwa mara kulikuwa na vita vingi huko. Wakati askari wa Yerusalemu waliposhinda vita, walitembea kuingia mjini humo. Viongozi wao waliwatangulia mbele wakiwa wamepanda farasi. Watu waliwafuata wakitembea kandokando ya njia na kupaza sauti zao kuhusu habari za vita. Viongozi walisifiwa sana kwa ushujaa wao. Wakati huo ulikuwa wakati wa furaha kwa sababu walishinda maadui zao.

Yesu alijua mila hii. Alijua kwamba watu wangeelewa maana yake. Alikata shauri kutumia mila hii ya zamani kuwafundisha watu kuwa yeye ni nani. Kwa hivyo, aliwatuma wafuasi wake kwenda kumchukua mwana-punda ambaye angesafiria. Angeingia mjini akiwa amempanda mwana-punda kama kiongozi. Wafuasi na wanafunzi wake wangemfuata nyuma kama jeshi lake. Kila mmoja angepaza sauti ya kumtukuza Mungu kwa kuwatumia mfalme. Yesu aliwatuma wanafunzi wake kumchukua mwana-punda. Alikuwa ni mwana-punda ambaye hakuwa amekwisha kupandwa na mtu ye yote. Hii ilionyesha kwamba Yesu alikuwa mtu wa aina ya kipekee.



kutambua sehemu yao ya kushiriki wokovu wao na vijana wengine. Labda wanaweza kumwambia rafiki yao mwanafunzi, au rafiki wanayecheza naye habari hiyo ya wokovu. Katika kila mahali kuna watu ambao hawajasikia habari njema ya kwmaba kuna wokovu kwa watu wote.

Omba kwamba tutaweza kuwa mashahidi wema wa wokovu ambao Kristo ametupa.

Sauti ilisema nini mara ya pili? — "Vilivyotakaswa na Mungu, usiite najisi."

Jambo hili lilitendeka mara ngapi? — Mara tatu

Petro alistaajabia maana ya maono haya. Alipokuwa akistaajabu, watu wale kutoka kwa Kornelio waliwasili.

Ni nani aliyemwambia Petro kufuatana na watu wale waliotumwa kwake na Kornelio? <u>ROHO MTAKATIFU</u>

Piga mstari chini ya sentensi inayoeleza mambo ambayo Mungu alimfundisha Petro.

Petro asikae na Kornelio kwa muda mrefu.

<u>Petro asimwite mtu ye yote mchafu wala najisi, kwa maana Mungu anampenda kila mtu.</u>

Soma Matendo 10:39-43. Sasa chora mviringo wa herufi "K" iliyo kando ya sentensi ya kweli, na uchore mviringo kwa herufi "M" iliyo kando ya sentensi ambayo si kweli (au makosa).

<u>K</u> M Tuliyaona mambo ambayo Yesu alifanya katika Uyahudi wote.

<u>K</u> M Wayahudi walimwua Yesu.

<u>K</u> M Mungu alimfufua Yesu siku ya tatu katika wafu.

K <u>M</u> Halafu kila mmoja katika Yerusalemu alimwona Yesu.

<u>K</u> M Yesu alituagiza sisi kuhubiri na kushuhudia habari zake.

<u>K</u> M Kila amwaminiye Yesu atapata ondoleo la dhambi.

## KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

**"Huyo (Yesu) manabii wote humshuhudia, ya kwamba kwa jina lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi." Matendo 10:43.**

Manabii wa Agano la Kale waliandika habari za kuja kwake Yesu kuwaokoa watu katika dhambi zao. Petro aliona ya kwamba Mungu anampenda kila mtu. Mungu anataka kila mmoja kuokolewa. Lakini, watu wale tu wanaomwamini Yesu ndio wanaosamehewa dhambi zao. Mungu hajali rangi ya mtu. Mungu hajali lugha ya mtu kwa sababu yeye ni Bwana wa watu wote. Ujumbe wa wokovu ulitolewa kwa watu wote. Petro alitambua kwamba ujumbe huo ulikusudiwa Watu wa Mataifa na Wayahudi. Yesu alishuka duniani kuja kwa ajili ya dhambi za ulimwengu, na ulimwengu unahusu watu wote.

## WAKATI WA KUFUNGA

Labda utapenda kufunga darasa kwa kukaza tena ukweli ule ambao Petro alijifunza kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya watu wote. Mara nyingi, vijana hawatambui ya kwamba wao pia ni wajumbe wa habari hii njema. Unaweza kuwasaidia wanafunzi wako



**Hapakuwapo mfalme kama yeye, na hakutakuwapo tena. Alikuwa Mwokozi wa pekee, Masihi mmoja aliyeahidiwa na Mungu.**



Yesu aliwaambia wanafunzi wake jinsi ya kujibu kama mtu angewauliza kwa nini walimchukua mwana-punda. Waseme kwamba Yesu ndiye alimhitaji mwana-punda yule.

Mwulize mwanafunzi mmoja asome Luka 19:32-34. Yesu alijua mambo yote. Bila shaka wanafunzi waliona ajabu tena kwa uwezo mkuu na hekima ya Yesu. Kila kitu kilitendeka kama alivyosema.

Soma Luka 19:35-36. Yesu aliingia Yerusalemu kama mfalme. Desturi ya wafalme ilikuwa kupanda farasi mkubwa wa vita, lakini Yesu alipanda mwana-punda, mnyama wa amani. Yesu alitumia jambo hili kama dalili. Ufalme wake haungekuwa ufalme wa kijeshi. Ungekuwa ufalme wa amani.

**Wanafunzi hawakuwa na tandiko zuri ya kutandika juu ya mwana-punda. Walitumia nguo zao kumtandikia Yesu juu ya mwana-punda. Wengine walitandaza nguo zao njiani. Walitaka watu wote wajue ya kwamba Yesu alikuwa mfalme wao, Masihi.**

**Soma Luka 19:37-38. Yesu alikuwa ameukaribia mji. Watu walijaa kila mahali. Wakati Yesu alipokuwa akisafiri juu ya mwana-punda, watu walianza kuwauliza wanafunzi wake kwamba yeye alikuwa nani. Wanafunzi walieleza kuhusu miujiza ya Yesu. Waliwaambia watu hao ya kwamba Yesu alikuwa mfalme. Waliamini kwamba alikuwa Masihi aliyeahidiwa kuja. Watu walifurahi sana waliposikia jambo hili. Walifikiria askari wa Kirumi ambao waliwaamuru jambo la kutenda. Walifikiria juu ya kodi ambayo walilipa serikali ya Kirumi. Walifurahi kuwa na Masihi ambaye angefanya hali ya maisha yao kuwa rahisi. Kwa hivyo, wao pia walianza kupiga makelele na kumtukuza Mungu.**

**Lakini si kila mtu alikuwa na furaha. Viongozi wa dini walisikia kelele, wakaenda kuona jambo ambalo liliwafanya watu kupiga kelele. Walipomwona Yesu akiingia mjini kama mfalme, walikasirika sana. Hawakuamini kwamba Yesu ndiye aliyekuwa Masihi. Hawakufurahi wakati Yesu alipowafunulia makosa yao. Walimwogopa Yesu kwa sababu alifanya mambo ambayo wao**

hawakuweza kufanya. Katika Luka 19:39 twasoma vile walivyomwambia Yesu. (Mwulize mwanafunzi mmoja akisome kifungu hiki.)

Sasa soma Luka 19:40. Yesu aliwapa Mafarisayo jibu la maana. Aliwaambia kwamba kama watu hao wangenyamaza, mawe ambayo yalikuwa kando kando ya njia ile yangepiga makelele. Yesu alijua kwamba ulikuwa wakati sasa kwa ulimwengu wote kujua kwamba yeye ndiye aliyekuwa mfalme na Mwokozi wao.

Bila shaka moyo wa Yesu ulijaa furaha kwa sababu alisikia watu wakimtukuza Baba yake wa mbinguni. Lakini katika kifungu cha 41 twasoma ya kwamba alikuwa na huzuni pia. Yesu alijua jambo ambalo lingetendeka mwishoni mwa juma lile. Alijua kwamba watu wangemkana. Wangempigia Pilato makelele atoe amri Yesu ahukumiwe kusulibiwa. Yesu alijua kwamba kifo chake kilikuwa lazima. Lakini pia alijua kwamba kifo chake kingekuja kwa sababu ya kutoamini kwa watu. Hawangefahamu kwamba ufalme wake ulikuwa wa Roho. Hiyo ndiyo sababu iliyomfanya kulia.

**KAZI YA KUFANYA**

Soma Luka 19:28-31. Weka alama hii ( X ) kwenye mistari iliyo kando ya mafungu ya maneno ambayo ni kweli.

__X__ Yesu alikuwa akienda Yerusalemu.

_____ Yesu alipitia mlima wa Kilimanjaro alipokuwa akienda Yerusalemu.

_____ Yesu aliwatuma wanafunzi wake sita wakamchukue mwana-punda wamletee.

_____ Mwana-punda yule alikuwa amekwisha kupandwa mara nyingi.

_____ Yesu alimpanda mwana-punda kwa sababu alikuwa amechoka kutembea.

__X__ Yesu alimpanda mwana-punda kwa sababu alitaka kuwaonyesha watu kwamba alikuwa mfalme wao.

Baada ya kusoma Luka 19:32-34, jaza sehemu zilizoachwa kwa kutumia maneno yaliyo sawa ili ukamilishe sentensi zifuatazo.



Wale waliotumwa wakaenda

<u>wakaona</u> kama <u>alivyowaambia</u>.

Na walipokuwa <u>wakimfungua</u>

mwana-punda, <u>wenyewe</u>



alivyokufa msalabani, akafufuka tena siku ya tatu, na baadaye akaonekana na watu wengi. Aliwaambia kwamba Kristo aliwaamuru kwenda katika nchi zote na kuwahubiria watu wote habari njema. Jambo moja kati ya maneno ambayo Petro aliyasema ni kifungu chetu cha kukumbuka cha leo. (Matendo 10:43) Katika Agano lote la Kale tunaona manabii wakifundisha kwamba siku moja mwokozi angekuja kuondoa dhambi za ulimwengu. Yesu huyu ndiye yule waliyetangaza habari zake.

Mtu anayemwamini Kristo husamehewa na Mungu dhambi zake zote. Kuwa Mkristo ndilo jambo moja la ajabu zaidi kuliko jambo lo lote ambalo mtu anaweza kufanya.

Kabla ya Petro kumaliza kusema, watu wale waliokuwamo nyumbani mwa Kornelio walifungua mioyo yao kwa Mungu wakamwamini Yesu ndiye alikuwa Kristo. Kisha Roho Mtakatifu aliwashukia wote, akiwathibitishia Wayahudi kwamba Mungu alitaka kuwaokoa watu wa Mataifa yote pia, wala sio Wayahudi peke yao.

Petro aliwaambia kubatizwa kama ishara kwa wengine ya kwamba walimpokea Yesu kama Mwokozi wao.

**KAZI YA KUFANYA**

Kornelio alikuwa akida wa jeshi la Warumi. Chora mstari kutoka kwa picha yake hadi kwa kila sentensi ya kweli.

Kornelio alimcha Mungu na kumpenda.



Aliwapa maskini pesa.

Alimwona malaika wa Mungu katika maono.

Hakumwogopa malaika huyo.

Aliambiwa Mungu alikuwa amekwisha kusikia maombi yake.

Aliambiwa kuwatuma watu kwenda kumwita Petro.

Aliwatuma watumishi wake wawili na askari kwenda Yafa.

Yeye mwenyewe aliondoka, akaenda kumlaki Petro.

Petro pia aliona maono. Chora mstari kutoka kwa kila swali hadi jibu lake.

| | |
|---|---|
| Petro aliomba wapi? | "Ondoka, Petro, uchinje ule." |
| Petro aliumwa na nini? | Jua darini |
| Aliona nini ndani ya nguo ile kubwa? | Njaa |
| Sauti ilimwambia nini? | Wanyama, nyoka na ndege |
| Petro alijibu nini? | "Hasha, Bwana" |

Wayahudi walikatazwa kula waliitwa najisi.

Petro alisema ya kwamba hangeweza kula wanyama kama hao. Lakini sauti ilimjia mara ya pili, ikamwambia, "Vilivyotakaswa na Mungu, usiviite wewe najisi." (Matendo 10:15) Jambo hili lilitendeka mara tatu kisha nguo ile kubwa na wanyama ndani yake ikatoweka.

Petro alisema, "Mimi ndiye mnayemtafuta. Mmekuja kwa sababu gani?"



Petro alipokuwa akistaajabia maana ya maono hayo aliyoyaona, watu wale waliotumwa na Kornelio kwake waliwasili. Roho Mtakatifu alimwambia Petro kufuatana na watu wale kwa sababu Mungu ndiye aliyewatuma kwake. Petro alishuka mara moja, akasema na watu wale, akawakaribisha wawe wageni wake.

Petro alikuwa na nia ya kwenda pamoja na watumishi wale wa Kornelio kwa sababu Mungu alikuwa amekwisha kutayarisha moyo wake kwa maono. Siku ya pili, asubuhi, Petro na Wayahudi wengine na watumishi wale wa Kornelio walianza safari ya kwenda Kaisaria.

Walipofika, Kornelio alitoka mbio kuja kumlaki Petro, akamwangukia miguuni, akamsujudia. Petro alimwambia Kornelio asimsujudie yeye, bali amsujudie Mungu tu. Yeye alikuwa tu mtumishi wa Mungu. Petro alipoona ya kuwa Kornelio aliwakusanya jamaa zake na marafiki zake zote, alifahamu kabisa jambo ambalo Mungu alikuwa akijaribu kumwambia kwa maono aliyoyaona. Aliwaambia watu hao: "Ninyi mnajua ya kuwa si halali mtu aliye Myahudi ashikamane na mtu aliye wa taifa lingine wala kumwendea, lakini Mungu amenionya, nisimwite mtu awaye yote mchafu wala najisi. Kwa sababu hiyo nalikuja nilipoitwa nisikatae; basi nawauliza, ni neno gani mliloniitia?" Matendo 10:28-29.

Kisha Kornelio alisimulia juu ya maono yake aliyoona, kisha akasema, "Basi sasa sisi sote tupo hapa mbele za Mungu, tupate kuyasikiliza maneno yote uliyoamriwa na Bwana." (Matendo 10:33)

Petro alianza kwa kusema kwamba sasa alielewa ya kwamba Mungu hapendi mtu mmoja kuliko mwingine. Wale wanaokubaliwa na Mungu ni wale wanaojaribu kumpendeza Mungu na ambao maisha yao yanaonyesha kwamba wanamwamini Yesu.

Petro aliendelea kuwaambia watu wale habari za Yesu na jinsi



waliwaambia, "Mbona mnamfungua

mwana-punda?" Wakasema

"Bwana ana haja naye.

Andika maneno ambayo watu walisema kuhusu Yesu katika mstari wa 38.

Wakasema, ndiye mbarikiwa mfalme ajaye kwa jina la Bwana, amani mbinguni, na utukufu huko juu.

Soma Luka 19:41, ili upate majibu sawa ya maswali yafuatayo. Kisha, piga mstari chini ya maneno ambayo wafikiri yatakamilisha maana ya sentensi hizo.

Yesu alililia Yerusalemu kwa sababu

a) aliwapenda wenyeji wa Yerusalemu.

b) hakuupenda mji ule.

Yesu alilia kwa sababu alijua

a) watu wengi hawakumwamini.

b) aliumia mguu.

Yesu alilia kwa sababu

a) alitaka kuishi mioyoni mwa watu, na alijua ya kwamba hawakumwelewa.

b) alisikia jasho na kiu.

Waweza kuandika majibu mafupi ya maswali yafuatayo?

Kwa nini Yesu aliingia mjini akiwa juu ya mwana-punda badala ya kutembea kwa miguu kama ilivyokuwa kawaida yake?

Kuwafundisha watu kuwa Yeye alikuwa nani.

Ni aina gani ya ufalme ambao Yesu alitaka kuleta? Ufalme wa amani na upendo.

Ufalme huo wapatikana wapi? Katika mioyo ya watu.

Kwa nini Yesu alijaribu kuwafundisha wafuasi wake wafanye kazi yake? Kwa sababu angewaacha baada ya muda mfupi.

Je, Yesu aishi maishani mwako sasa? ________________

**KIFUNGU CHA KUKUMBUKA**

**"Wakasema, Ndiye mbarikiwa Mfalme ajaye kwa jina la Bwana; amani mbinguni, na utukufu huko juu." Luka 19:38**

**WAKATI WA KUFUNGA**

Waambie wanafunzi wainamishe vichwa vyao. Waulize ikiwa wanaamini katika ufalme wa Mungu. Waulize ikiwa wanaamini mioyoni mwao, au ikiwa wanaogopa kufikiri kuhusu Mungu. Omba ya kuwa Mungu awe katika maisha na moyo wa kila mmoja wao.

# YESU ALIKULA NA WANAFUNZI WAKE

**MASOMO YA BIBLIA: Luka 22:7-23**

**KUJIANDAA KUFUNDISHA**

Yesu alitupa amri chache sana. Sisi twaamini kwamba alilipa kanisa maagizo mawili. Moja kati ya haya ni "Ubatizo". Lingine lilikuwa "Meza ya Bwana". Funzo hili litahusika na Meza ya Bwana, historia yake, na maana yake.

Mara kwa mara Yesu alitumia katika mithali yake mambo ambayo watu waliyaona kila siku wakati yeye na wanafunzi wake walipokuwa wakizunguka huku na huku kufundisha mambo ya kiroho. Mithali yake ilikuwa juu ya kupanda mbegu, kwenda katika safari, au kuchunga kondoo. Yesu alitumia Sikukuu ya Kiyahudi ya Pasaka kufundisha mambo ya kiroho. Alibadilisha jina la Sikukuu hiyo, akawapa Kanisa Meza ya Bwana (au Chakula cha Bwana).

Na tuiangalie karamu ya Pasaka ili tuweze kuelewa kwa ukamilifu maana ya karamu mpya ambayo Yesu aliitoa. Waisraeli walikuwa wameishi Misri tangu Yusufu alipohamia huko kuikimbia njaa. Baadaye walilazimishwa kuwafanyia Wamisri kazi kama watumwa. Wakiwa katika maisha hayo magumu, Waisraeli walimwomba Mungu msaada. Mungu aliyasikia maombi yao. Alimtuma Musa kwenda kumwambia Farao wa Misri kuwaruhusu Waisraeli waondoke Misri. Mungu alituma misiba kumi kumshawishi Farao kwamba ilikuwa lazima amtii Mungu.

Usiku wao wa mwisho huko Misri, Waisraeli waliamriwa kuchinja mwana-kondoo na kupaka damu yake kwenye milango yao. Kisha wale nyama ya mwana-kondoo yule pamoja na mikate isiyotiwa chachu. Mungu angeonyesha uwezo wake usiku ule na Waisraeli wangeondoka Misri kwa haraka. Hakungekuwa na wakati wa kuiacha mikate hadi itakapovimba. Watu waliomwamini Mungu walifanya kama walivyoambiwa. Malaika wa kifo alipopitia Misri usiku ule, mzaliwa wa kwanza katika kila nyumba ya Mmsri aliuawa. Lakini pale ambapo mwana-kondoo alichinjwa, na damu yake kupakwa milangoni, mzaliwa wa kwanza hakuuawa. Mwana-kondoo alikuwa amekufa badala yake.

Mungu aliwaamuru watu waiadhimishe karamu hii kila mwaka kukumbuka vile aliwatoa Misri. Ilikuwa karamu ya ukumbusho.

Wakati wa karamu hii ulikuwa umekaribia Yesu alipokwenda Yerusalemu. Aliipa karamu hii jina mpya. Alijiita yeye mwenyewe mwana-kondoo. Aliwaambia wanafunzi wake ya kwamba angeuawa badala ya watu walio na dhambi. Pia, Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba iliwapasa kuila karamu hii lakini hakusema



alyeahidiwa kuja, ndio waliokuwa Wakristo. Kwanza, waamini wa Kiyahudi walishika sheria zile maalum zao walizozishika tangu wakati wa Musa. Kwa mfano hawangeweza kula chakula cha aina fulani. Na hawangeweza kwenda nyumbani mwa watu wa Mataifa.

Wayahudi walifikiri ya kwamba Mungu aliwapenda zaidi kuliko vile anavyowapenda watu wa Mataifa. Tena, wao ndio waliokuwa watu waliochaguliwa na Mungu.

Hebu sasa tumwone mtu huyu wa Mataifa aliyempenda Mungu. Kornelio alikuwa akida katika jeshi. Alisimamia kikosi cha askari mia moja. Kikosi hiki kilikuwa cha askari wa Kiitalia, na

pengine kilikuwa cha kumlinda liwali. Mji wa Kaisaria uliokuwa katika pwani ya Bahari ya Kati, ulikuwa mji mkubwa sana. Ulikuwa bandari muhimu kwa wakuu wa Kirumi waliotumwa kuja kutawala Uyahudi (Palestina).

Kaisaria ulikuwa mji wenye ulinzi mkali, na ulijengwa tena na Herode na ukapewa jina la Mfalme Kaisari Augusto kama heshima na ukumbusho wake.

Kornelio alimwabudu Mungu wa Wayahudi. Alijaribu kufanya mambo ambayo alifikiri Mungu alimtaka kufanya. Aliwapa maskini pesa na kumwomba Mungu daima. Kwa sababu Mungu alijua jinsi Kornelio alimpenda na jinsi alitaka kumtumikia, siku moja alisema naye katika maono. Ilikuwa yapata saa tisa ya mchana, wakati uliokuwa wa kawaida kwa Wayahudi kuomba.

Kwanza, Kornelio alishangaa sana, kisha, bila shaka alifurahi wakati malaika alipomwambia ya kwamba Mungu alikumbuka sala zake. Halafu malaika alimwambia kuwatuma watu kwa Petro ambaye alikuwa akikaa katika nyumba ya Simoni mtengenezaji wa ngozi katika Yafa.

Kornelio aliwatuma watumishi wake wawili na askari kwenda kwa Petro kumwambia aje. Kama saa sita ya mchana siku ya pili yake, watu wale waliotumwa na Kornelio kwa Petro walikuwa wamekaribia mji wa Yafa. Wakati walipokuwa wakiingia njini, Petro alikuwa juu darini akiomba. Nyumba za mji ule zilikuwa na dari tambarare. Kwa hivyo watu waliweza kukaa humo na kupunga upepo. Petro alikuwa akingojea chakula cha mchana kuandaliwa na alikuwa akisikia njaa sana. Kwa ghafula aliweza kusikia ujumbe wa Mungu, wa ajabu kwake.

Aliona maono, na katika maono hayo aliona chombo kama nguo kubwa ikitelemshwa kutoka mbinguni kwa pembe zake nne. Ndani yake walikuwamo aina zote za wanyama na ndege. Wakati nguo hiyo ilipokuwa ikitelemshwa, sauti ilisema, "Ondoka, Petro, uchinje ule."

Bila shaka Petro alikuwa na njaa sana, lakini alitazama nguo hiyo kwa makini, akaona kwamba ndani yake walikuwamo aina zote za wanyama. Wakati huu, Wayahudi walikuwa tu chakula ambacho kiliruhusiwa na sheria za Musa. Wanyama ambao

Sura ya Kumi na Mbili

# WATU WA MATAIFA WASIKIA HABARI ZA WOKOVU

**MASOMO YA BIBLIA: Matendo 10**

**KUJIANDAA KUFUNDISHA**

Soma Warumi 10:12-13. Vifungu hivi vinaonyesha kwamba wokovu ni kwa watu wote, kwa watu weusi, weupe, na wekundu. Ni kwa makabila yote na mataifa yote. Je! hii maana yake kwamba Mungu anapenda Kenya na Amerika, Wajaluo na Wakikuyu, Tanzania na Afrika Kusini kwa upendo mmoja? Ndiyo. Katika maandiko ya somo hili, Matendo 10: 34-35, tunasoma ya kwamba "Mungu hana upendeleo; bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na yeye."

Kusudi la somo hili ni kuonyesha kwamba wokovu wa Mungu ni kwa watu wote. Kusudi hili pia ni kuwasaidia vijana kutambua ya kuwa wao pia wana wajibu wa kuwaambia wengine habari za upendo wa Yesu.

**MAMBO YA KUKAZA**

1. Kornelio alimcha Mungu hata kabla ya kuwa Mkristo.

2. Bwana alimwongoza Kornelio kwa Petro ambaye angemsaidia na kumwongoza kumjua Mwokozi.

3. Mungu alimtumia maono kumtayarisha Petro kuwaletea watu wa Mataifa habari yake njema.

4. Roho Mtakatifu alimwonyesha Petro ya kwamba Mungu alikuwa amekwisha kuwapokea waamini wapya wa Mataifa.

5. Sisi pia inatupasa kutafuta nafasi za kushiriki ujumbe wa Kristo na watu wasio wa kabila letu, wa jamaa yetu, au wa taifa letu.

**KULIFUNDISHA SOMO**

(Sema:) Hebu fikiria mtu ambaye humpendi. Labda mtu huyu yumo darasani mwenu shuleni, au pengine ni jirani yako wa kabila tofauti na lako. Mtu huyu ni mgeni kwako na hujali kufanya urafiki naye. Je! unafikiri Mungu anaweza kukupenda wewe rahisi zaidi kuliko vile anavyoweza kumpenda mtu huyu? Petro alifikiri Mungu angeweza kumpenda yeye rahisi zaidi kuliko vile angeweza kuwapenda watu ambao hawakuwa Wayahudi.

Mpaka wakati huu, karibu wale wote ambao walikwisha kumpokea Yesu kuwa Mwokozi wao walikuwa Wayahudi. Sasa ilimpasa Petro kujua kwamba habari njema ya wokovu ilikusudiwa watu wote, wala sio Wayahudi peke yao.

Wayahudi walikuwa watu maalum wa Mungu kwa sababu Mungu alikuwa amekwisha kuwapa ulimwengu amri zake kwa njia ya Wayahudi. Pia Mungu alitimiza ahadi yake ya kumtuma Masihi ulimwenguni kwa Wayahudi.

Wayahudi tu ambao waliamini kwamba Yesu alikuwa Masihi



mara ngapi. Alisema ya kuwa divai ilikuwa dalili ya damu yake. Mkate uliku wadalili ya mwili wake. Karamu hii huwakumbusha Wakristo kuhusu Agano Jipya la Mungu. Kusudi la somo hili ni kuonyesha kwamba, ikiwa watu watamwamini Yesu kama mwana-kondoo wao, na kuamini kwamba damu yake itawaokoa, Mungu atawasamehe dhambi zao wakati atakapowahukumu watu wote. Hii ndiyo maana ya Meza ya Bwana.

**MAMBO YA KUKAZA**

1. Yesu alitumia mambo ya kawaida kufundisha mambo ya kiroho.

2. Yesu alikufa badala ya kila mtenda dhambi, kama vile mwana-kondoo alivyokufa badala ya wazaliwa wa kwanza wa Israeli.

3. Meza ya Bwana ni wakati wa kukumbuka kifo cha Yesu.

4. Divai yatukumbusha damu ya Yesu.

5. Mkate watukumbusha mwili wa Yesu.

6. Yesu alituambia tuadhimishe Meza hii ya Bwana. Ni moja kati ya agizo la Kanisa

**KULIFUNDISHA SOMO**

Somo letu la leo laanza na hadithi ya sikukuu ya zamani. Je, wapenda sikukuu? Waweza kuniambia kuhusu sikukuu iliyopita siku chache zilizopita na ukaifurahia? (Toa wakati kwa mazungumzo. Watie wanafunzi moyo kukumbuka furaha, wageni maalum, au chakula cha sikukuu.)

Na tufungue somo letu linalohusu Meza ya Bwana. Somo hili linakueleza vile Yesu alikichukua chakula cha karamu na kukifanya kuwa na maana mpya. (Anza kueleza hadithi kwa njia hii)

Yesu alikuwa katika Yerusalemu. Wakati wa karamu ya Pasaka ulikuwa umekaribia. Kila jamaa walikuwa wakinunua mwana-kondoo. Kila mama alichunguza kwa makini katika kabati yake kuona kwamba hakusahau kununua cho chote ambacho kingehitajika kwa ile karamu. Watoto walisalimiana kwa haraka wakati walipokuwa wakienda dukani au sokoni kuvinunua vitu. Kila mtu alitembea kwa haraka na kucheka mara kwa mara kwa furaha. Watu waliokuwa wamehama, walirejea nyumbani kuwaona jamii zao. Kila mtu alionekana kuwa mwenye furaha. Kila mtu aliendelea kujitayarisha.

Je, hii ni sawa na vile mnavyosherehekea sikukuu katika mji wako? Je, watu wa mji wako hujitayarisha kwa sikukuu? Hii ilikuwa siku kuu ya kidini. Inaweza kuitwa siku takatifu. Ulikuwa wakati wa kukumbuka vile Mungu alivyokuwa amewasaidia Wayahudi miaka mingi iliyopita. Jamaa walipoketi chini kula karamu, baba wa jamaa alisimulia hadithi juu ya sikukuu ya kwanza ya Pasaka. Watoto walipendelea sana hadithi, na walipenda kuisikiliza hadithi hii.

Miaka mingi sana iliyopita, wana wa Israeli waliishi Misri. Walikuwa watumwa na mara nyingi waliomba kwamba Mungu angewasaidia katika shida zao. Mungu alimtuma Musa kwenda kuwasaidia. Musa alikwenda, akasimama mbele ya kiti cha enzi cha Farao. Alimwambia Farao ya kwamba Mungu aliwataka Waisraeli, wanaoitwa sasa Wayahudi, waondoke Misri. Farao aliifikiria kazi yote ambayo Waisraeli waliifanya. Alisema kwamba hawawezi kuondoka. Mungu alileta misiba tisa juu ya nchi ya Misri kumwonyesha Farao uwezo wake ili Farao angemtii. Lakini Farao aliendelea kusema, "Haiwezekani!"

Kisha Mungu alimwambia Musa habari kuhusu msiba wa kumi ambao alipanga kuleta juu ya Wamisri. Wazaliwa wote wa kwanza wa kiume wa Wamisri wangeuawa usiku ule. Katika nyumba ambamo watu walimwamini Mungu, palikuwa na njia ya kuwaokoa wazaliwa wa kwanza. Kila jamaa waliambiwa kumchinja mwana-kondoo na kupika nyama yake kwa chakula cha jioni. Waliambiwa kuchukua damu ya mwana-kondoo huyo na kupaka kwenye milango yao. Walitengeneza mikate isiyotiwa chachu. Hii ilionyesha kwamba walipaswa kuondoka Misri mara moja. Mungu alijua kwamba wakati huu Farao hangekataa kuwapa ruhusa kuondoka, bali angekubali.

Mambo yalitendeka kama Mungu alivyosema. Wakati wa usiku, malaika wa Mungu (wa kifo) alipitia Misri. Katika kila nyumba ambayo ilikuwa na damu mlangoni, malaika alipita bila kuingia ndani na kuleta uharibifu wo wote. Wazaliwa wa kwanza wakasalimika. Mwana-kondoo alikuwa amekufa badala yao. Lakini katika nyumba nyingine, vilio vilisikika, kwa kuwa wazaliwa wa kwanza waliuawa.

Waisraeli waliambiwa waondoke Misri mara moja! Majirani zao waliwapa zawadi, na kuwaomba waondoke. Kwa hivyo wakaondoka Misri. Waliacha kazi zao kama watumwa. Mungu alikuwa amewasaidia. Mungu hakutaka Waisraeli wasahau. Musa aliwaambia ya kwamba Mungu aliwataka kuadhimisha karamu hii kila mwaka kukumbuka vile Mungu aliyajibu maombi yao. Iliwabidi kumchinjia mwana-kondoo na kukumbuka vile malaika wa Kifo alivyowaacha wazaliwa wao wa kwanza. Wakati mwingine karamu hii iliitwa Karamu ya Mkate Usiotiwa Chachu. Mara nyingine iliitwa Karamu ya Pasaka.

Na tusome katika vitabu vyetu hadithi juu ya Pasaka. Vifungu hivi vinatuambia kwamba Yesu pia alikuwa akijitayarisha kwa karamu hii. Aliwatuma Petro na Yohana kwenda kutayarisha chumba na pia kutayarisha chakula.

Mwulize mwanafunzi mmoja asome Luka 22:7-8. Sasa soma Luka 22:9-13.

Wanafunzi wa Yesu hawakuwa na nyumba mjini Yerusalemu. Walimwuliza Yesu ikiwa wangekipata wapi chumba. Yesu aliwapa dalili. Aliwapa kazi ya kufanya lakini





2. Filipo alimbatiza Mkushi.

3. Walipopanda kutoka majini, Roho wa Bwana alimnyakua Filipo.

4. Mkushi alimwona Filipo kesho yake katika njia ile ya jangwani.

5. Mkushi alikwenda zake akifurahi.

6. Kisha Filipo alihubiri habari za Yesu katika miji mingine.

**KIFUNGU CHA KUKUMBUKA**

**"Uniendeshe katika mapito ya maagizo yako, Kwa maana nimependezwa nayo."**
**--- Zaburi 119:35**

**WAKATI YA KUFUNGA**

Sasa mjifunze pamoja na wanafunzi wako kifungu cha kukumbuka cha leo.

Funga darasa kwa maombi ya kwamba Mungu atamfanya kila mmoja wetu kugundua na kufanya mapenzi ya Mungu mara moja bila kuuliza swali.

Je! alizungumza habari za nani?

Stefano Musa Yesu

Je! ni kitu kipi kingine alichokifanya?

Alilisha umati wa watu | Aliimba | Aliponya wagonjwa

Mtu mmoja katika nchi ya Samaria, ambaye aliitwa Simoni, alifanya uchawi. (Matendo 8:9-13) Chora mstari chini ya sentensi za kweli kuhusu Simoni.

Alifanya uchawi mjini.

Watu walimwita, "Uweza wa Mungu, ule mkuu".

Aliwapa maskini pesa.

Alipomsikia filipo akihubiri alimwamini Kristo.

Soma Matendo 8:18-22 upate kuona ni kwa nini Petro alimkemea Simoni.

Je! Simoni alitaka kuwapa mitume kitu gani kama wangempa uwezo wa Roho Mtakatifu? PESA

Je! uwezo huu mkuu ungeweza kununuliwa? HAPANA

Petro alimwambia Simoni ya kwamba MOYO wake haukuwa mnyofu mbele za Mungu.

Soma Matendo 8:26-28. Tazama uone mahali ambapo Bwana alimtaka Filipo kwenda. Weka alama hii ( X ) kando ya sentensi zilizo kweli.

_X_ Malaika wa Bwana alimtuma filipo kwenda upande wa kusini wa jangwa la Gaza.

_X_ Filipo alikutana na mtu wa Kushi njiani ambaye aliwekwa juu ya hazina yote ya malkia.

____ Mkushi huyo alikuwa akiimba wakati alipokuwa akitembea njiani.

_X_ Alikuwa akisoma hati ya kuvingirisha ya nabii Isaya.

Soma katika Matendo 8:29-34 uone jinsi Filipo alipokimbia kwenda kukutana na mtu yule aliyekuwa ndani ya gari. Andika mambo waliyoyasema wote wawili.

Filipo: Je! yamekuelea haya unayosoma?

Mtu wa Gari: Nitawezaje kuelewa, mtu asiponiongoza?

Filipo alimwambia mtu yule ya kwamba Yesu ndiye yule ambaye manabii wa Agano la Kale walisema angekuja. Yesu, Mwana wa Mungu, alikuja kutoka mbinguni kutuokoa katika dhambi zetu. (Matendo 8:35-37) Je! mtu yule alifanya nini kuonyesha kwamba alimwamini Yesu kwa moyo wake wote?

Alimwuliza Filipo kumbatiza.

Filipo alimbatiza.

Soma katika Matendo 8:38-40 ya kwamba Filipo na Mkushi, wote walifurahi kwa kuwa Filipo alimtii Mungu. Weka alama hii ( X ) katika picha ya moyo iliyo kando ya kila sentensi ya kweli.

1. Filipo alimwambia Mkushi kuingia majini peke yake.



akawasaidia kuifanya! Waliambiwa wamtafute mwanamume aliyebeba mtungi wa maji. Hili lilikuwa jambo lisilokuwa la kawaida. Kwa kawaida wanawake tu ndio waliobeba mtungi wa maji.

Petro na Yohana walipomwona mwanamume aliyebeba mtungi wa maji, walimtii Yesu na kumfuata. Pengine mwanamume yule alikuwa anabeba maji kwa sababu alikuwa mtumishi. Wakati alipoingia nyumbani, Petro na Yohana pia waliingia mle. Walimwuliza mwenye nyumba kuwapa chumba. Walimweleza kwamba Yesu alihitaji pahali pa kula karamu pamoja na wanafunzi wake. Mwenye nyumba aliwaonyesha chumba cha juu (orofani). Aliwaambia kwamba Yesu angeweza kula karamu na wanafunzi wake katika chumba kile. Kwa hivyo, Petro na Yohana walitayarisha kila kitu.

Sasa soma Luka 22:14-16. Wanafunzi wote walikuwa katika chumba cha juu (yaani orofani) pamoja na Yesu. Yesu alikuwa amewafundisha na kusafiri pamoja nao kwa miaka mitatu. Aliwapenda. Alitaka kuwa pamoja nao kwa mara hii ya mwisho.

Yesu alijua kwamba kufa kwake kulikuwa karibu sana. Aliwaambia wanafunzi wake kwamba ilikuwa imebaki siku chache tu kisha angeteswa. Mambo yalikuwa yakifanyika kulingana na mpango wa Mungu kwa kuja kwa ufalme wake. Yesu aliwaambia wanafunzi hao kwamba hangekula nao tena.



Mwulize mwanafunzi mmoja asome Luka 22:17-20.

Yesu alichukua sehemu ya chakula mezani. Kulikuwa na divai. Kulikuwa pia na mkate usiotiwa chachu. Yesu alivichukua vitu hivi vya kawaida na kuvipa maana mpya. Yesu alikichukua kikombe, akakibariki, na akakipitisha kwa wanafunzi wote kumi na wawili. "Matunda ya mzabibu" ni njia moja ya kusema kwamba divai ile ilitoka kwa zabibu. Ilikuwa na rangi nyekundu. Iliwakumbusha wanafunzi kuhusu damu. Yesu aliwaambia kwamba divai ilikuwa dalili ya Agano Jipya la Mungu. Agano hilo lilihusu damu ya Yesu. Pia, Yesu alichukua sehemu ya mkate. Aliibariki na kumpa kila mmoja wao. Akawaambia, "huu ni mwili wangu ninaowapa. Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu."

Hii ilikuwa Meza ya kwanza ya Bwana. Yesu alikuwa anatufundisha jambo jipya. Alikuwa akionyesha kwamba yeye ndiye mwana-kondoo na kwamba sisi ndio wazaliwa wa kwanza. Yesu alikufa kwa ajili yetu. Twaweza kusamehewa dhambi zetu ikiwa tutaiamini damu ya Yesu kutuokoa.

Baada ya kuliamini agano hili, tunahitaji kuwa na Meza ya Bwana na kukumbuka kifo cha Yesu. Twatumia divai na mkate kutusaidia kukumbuka msalaba. Yesu alipokufa, wanafunzi wake walikumbuka kwamba Yesu alikuwa amewaambia kulifanya jambo hili. Hii ndiyo sababu tunashiriki Meza ya Bwana makanisani mwetu.

Soma Luka 22:21-23. Wanafunzi walikuwa bado wanafikiri kuhusu chakula hiki kipya. Maneno ya Yesu yaliyofuata yalikuwa ya kushangaza. Aliwaambia kwamba mmoja kati ya wale kumi na wawili angemsaliti. Wanafunzi wake walikuwa wameelewa kwamba Yesu alijua mambo hata kabla ya kutendeka. Walianza kuulizana wao kwa wao ni nani angemtendea Yesu vile. Hakuna hata mmoja aliyetaka kuwa msaliti. Lakini alikuwa Yuda.

Usiku ule ule Yesu alikamatwa. Baada ya muda mfupi angeonekana akiwa ameangikwa msalabani katika Fuvu la Kichwa. Wakati wake wa kufundisha ulikuwa umemalizika. Muda mfupi baadaye, ingekuwa wakati wa wanafunzi kuiendeleza kazi ya Yesu. Baada ya kusulibiwa na kufufuka, mpango wa Mungu wa kuleta wokovu kwa mwanadamu ungekamilika. Ujumbe wa Mungu kwa wanadamu ungetimia. Huu ndio ujumbe uliopewa kanisa. Ungehubiriwa ulimwenguni kote.

## KAZI YA KUFANYA

Jaza nafasi zilizoachwa kwa kutumia maneno ya kukamilisha sentensi zifuatazo.



Kila mtu katika Yerusalemu alifurahi, kwa sababu Karamu ya <u>Pasaka</u> ilikuwa inakaribia. Watoto waliwa<u>saidia</u> mama zao. Kila jamaa walihitaji <u>mwana-kondoo</u> kuchinja na kuchoma. Iliwapasa kuonyesha jinsi walivyoondoka <u>Misri</u> haraka kutotia <u>chachu</u> katika mikate yao.

Piga mstari chini ya jibu ambalo ni sawa.

1. Pasaka ilikuwa wakati wa

(a) kucheza michezo.

(b) <u>kukumbuka msaada wa Mungu kwa Israeli.</u>

2. Mwana-kondoo alichinjwa na kufa badala ya

(a) Farao.

(b) <u>wazaliwa wa kwanza wa jamii walioamini.</u>



unabii wa Agano la Kale juu ya Yesu. Aliona nafasi hii kuwa nzuri sana ya kushuhudia mtu huyu habari za Bwana.

Mtu huyu hakuelewa maandiko aliyokuwa akisoma. Kwa hivyo, alifurahi wakati filipo alipojitoa kumsaidia. Mtu anapomtafuta Bwana kweli, kwa kawaida huhitaji kusaidiwa na mtu anayempenda Bwana na anayejua maandiko. Sababu moja kubwa ya sisi kuja kwa Shule ya Jumapili ni kupata msaada katika kujifunza Neno la Mungu. Mtu huyu alikuwa akisoma maandiko haya kutoka Isaya 53:7-8.

"Alionewa, lakini alinyenyekea, wala hakufunua kinywa chake; kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni, na kama vile kondoo anyamazavyo mbele yao wakatao manyoya yake; naam, hakufunua kinywa chake. Kwa kuonewa na kuhukumiwa aliondolewa; na maisha yake ni nani atakayeisimulia? Maana amekatiliwa mbali na nchi ya walio hai; alipigwa kwa sababu ya makosa ya watu wangu."

Kisha, Filipo kwa kuanzia maandiko hayo, alimhubiria Yesu. Je! kama ingalikuwa wewe ungaliweza kujibu swali ambalo Mkushi alimwuliza Filipo? Aliuliza katika kifungu cha 34, "Nabii huyu asema maneno haya kwa habari ya nani?" Filipo aliweza kumjibu kwa sababu aliyajua maandiko, na tena alimjua Yesu. Labda Mungu hakukutumia wewe kwa sababu hujui Biblia, au pengine humjui yeye.

Hatujui ni kwa muda gani Filipo na Mkushi walikaa pamoja, lakini Mkushi alikuwa tayari kumwamini Mwokozi huyu wa ajabu ambaye alikuja kuteseka na kufa kwa ajili yake. Walipokuwa wakisafiri ndani ya gari lile, walifika mahali penye maji. Je! Mkushi alisema nini? (Mwambie mwanafunzi mmoja kusoma Matendo 8:36.) Mkushi alibatizwa, akaenda zake akifurahi. Alipofika katika nchi yao, bila shaka aliwaambia watu habari za Yesu. Ni jambo la kupendeza sana kwamba watu wengi wa Kushi walikuwa Wakristo tangu siku zile za kanisa, na wengi wanaamini kwamba mtu huyu (Mkushi) ndiye aliyekuwa wa kwanza kuleta Injili Afrika.

Baada ya Filipo kumbatiza Mkushi, Mungu alimnyakua, akampeleka mahali pengine ambapo watu walihitaji kusikia habari za Yesu.

Jambo kubwa linalotupasa kukumbuka juu ya Filipo ni kwamba hakutoa udhuru wakati Mungu alipomtuma, bali alimtii Mungu bila kumwuliza swali.

## KAZI YA KUFANYA

Tunasoma katika Matendo 8:5-8 ya kwamba mmojawapo wa marafiki wa Stefano walikwenda katika mji mkuu wa Samaria. Piga mstari chini ya maneno ya kweli kuhusu mhubiri huyu.

Je! mtu huyu alikuwa nani?

<u>Filipo</u>   Petro   Sauli

Filipo. Labda angalitoa udhuru mwingi asipate kwenda. Labda angalisema, "Bwana kuna joto jingi. Nitakwenda wakati jua litakapokuchwa." Au "Bwana, nimechoka sana kwa mahubiri yale niliyohubiri kwa ajili yako. Acha nipumzike kwanza kabla ya kwenda." Au "Bwana, sina mkuki, na labda huko jangwani kuna wanyama wakali. Vema nikae hapa ambapo ninaweza kuwashuhudia watu wengi bila hatari yo yote." Au "Bwana, jangwani hamna watu. Ni heri kunituma mahali pengine."

Mhubiri huyu mwaminifu hakutoa udhuru wo wote. Alimtii Bwana. Je! unafikiri Filipo alifikiria nini wakati alipokuwa akitembea katika njia ile jangwani? Labda alikuwa akistaajabu kwa nini Mungu alimtuma na hali alikuwa akitafuta nafasi ya kuhubiri habari za Mungu. Kisha aliona gari. Ndani ya gari lile mlikuwa na mtu mwenye mamlaka chini ya malkia wa Kushi.

Ingawa mtu huyu hakuwa Myahudi, alikuwa amekwenda Yerusalemu kumwabudu Mungu. Na sasa alikuwa akirejea kwao. Alipokuwa akisafiri ndani ya gari lile, alikuwa akisoma maandiko ya nabii Isaya.

Ni wazi kwamba mtu huyu alisikia habari za Mungu wa kweli na alitaka kumwabudu hasa. Basi, Mungu aliyeona tamaa hii moyoni mwake, alimtuma Filipo kwenda kumweleza njia nzuri ya kumjua Bwana.

Filipo alipoona gari lile, roho Mtakatifu alimwambia kusema na mtu huyu aliyekuwa ndani. Hapa tena Filipo alitii mara moja. Alikimbia kushikamana na gari lile. Akamwona mtu huyu akisoma. Ilikuwa desturi nyakati zile kusoma kwa sauti. Filipo, kwa kuwa alijua maandiko ya Agano la Kale, alifahamu mara moja kwamba maandiko ambayo mtu huyu alikuwa akiyasoma yalikuwa mojawapo ya





3. Damu ya mwana-kondoo ilipaswa

(a) kuzikwa karibu na mti.

(b) kupakwa mlangoni.



Weka alama hii ( X ) kuonyesha sentensi ambazo ni kweli na zisizo kweli.

Kweli Si kweli

X ____ 1. Yesu aliwatuma Petro na Yohana kwenda kuandaa karamu.

____ X 2. Petro na Yohana walimtafuta mtu aliyechukua kikapu cha mahindi.

X ____ 3. Nyama iliyopikwa katika karamu ilikuwa ya mwana- kondoo.

X ____ 4. Mkate haukutiwa chachu.

____ X 5. Petro na Yohana hawakumwona mwanamume aliyebeba mtungi wa maji.

X ____ 6. Kila kitu kilifanyika kama Yesu alivyosema.

Andika majibu sawa ya maswali yafuatayo.



Divai wakati wa karamu inatukumbusha damu ya Yesu.



Mkate wakati wa karamu unatukumbusha mwili wa Yesu.



Yesu aliwapa wanafunzi wake agano jipya.



Yesu alitwambia ya kwamba karama mpya ni ya kukumbuka kifo chake msalabani.

Baada ya Yesu kuondoka, kazi ya Mungu ingefanywa na wanafunzi wake.

**KIFUNGU CHA KUKUMBUKA**

**"Akatwaa mkate, akashukuru, akaumega, akawapa, akisema, Huu ndio mwili wangu." Luka 22:19**

**WAKATI WA KUFUNGA**

Someni pamoja kifungu cha Kukumbuka. Waambie wanafunzi kuinamisha vichwa vyao na kusikiliza kwa makini wakati unapowauliza maswali. Hawahitaji kuyajibu maswali hayo kwa sauti kubwa, lakini wayajibu kwa moyo.

Je, waamini kwamba damu ya Yesu inaweza kukuokoa? Je, waamini kwamba damu yake inaweza kumfanya Mungu akusamehe dhambi zako? Omba sasa hivi ili Mungu akusaidie uweze kuamini. Na tumshukuru Mungu kwa kumtuma Yesu kututayarishia njia ya wokovu. Tumshukuru Yesu kwa kufa msalabani badala yetu.

Toa nafasi kwa maombi ya kimya.

# YESU ANAHUKUMIWA NA KUSULIBIWA

**MASOMO YA BIBLIA: Luka 22:66- 23:56**

## KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wakati unapofundisha somo hili, <u>kusudi lako liwe la kuwasaidia wavulana na wasichana kuelewa kwamba Yesu alikufa kwa ajili yao.</u> Hakufa kwa sababu ilimpasa kufanya hivyo, lakini ni kwa sababu alitaka kutimiza mpango wa Mungu kwa kila mmoja wetu. Na mpango huu ulihusu kifo chake. Kama mtu angekuokoa ukiwa karibu kuzama katika mto, bila shaka ungefikiri kwamba una deni la maisha yako kwa yule mtu. Wasaidie vijana wadogo wafahamu kwamba, inawapasa kuchagua kuishi kwa Yesu ambaye alikufa kwa ajili yao.

Hakikisha kwamba wakati unapofundisha, unaeleza kwamba Yesu alikuwa na chaguo juu ya kufa msalabani au la. Je! unakumbuka maneno ya Yesu wakati alipoomba katika bustani kabla ya kushikwa kwake? "Ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke; walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe" (Mathayo 26:39). Maana ya maneno haya ni "Sitaki kufa msalabani, lakini ikiwa kufanya hivyo ni mapenzi yako kwangu, basi nitafanya hivyo."

Hukumu ya Yesu haikuwa ya haki. Kifo chake kilikuwa cha ukatili mno. Alifanya hivi ili kuchukua adhabu ambazo tunastahili sisi kwa ajili ya dhambi zetu. Yesu alipolia msalabani, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?" alikuwa akionyesha tisho ambalo hatuwezi kuelewa kwa ukamilifu. Yesu alitengwa na Mungu kwa wakati mfupi tu, lakini utengamano huu ulikuwa msiba wa kufa msalabani. Haikuwa tu maumivu makali ya misumari katika miguu na mikono yake, wala si haya ya kufa kama mhalifu, au si kama kiu kali. Utengamano huu na Mungu ulikuwa tisho kweli. Ikiwa tumechagua maishani mwetu kuishi kwa Yesu, basi kifo kitatuletea furaha kuu, kwa sababu tutakuwa na uhusiano na Mungu. Na ikiwa hatumchagui Kristo kama Mwokozi wetu, basi tutatengwa na Mungu milele.

## MAMBO YA KUKAZA

1. Kila mtu ni lazima achague kama atakuwa mfuasi wa Kristo au atakuwa adui wake.

2. Viongozi wa dini, makutano ya watu, na Pilato, wote walikuwa maadui wa Yesu.

3. Sisi, kwa sababu ya dhambi zetu, tu maadui wa Yesu mpaka tunapompokea kama Mwokozi wetu.

4. Wakristo ni lazima waonyeshe kwa matendo yao ya kila siku kwamba wao ni watu wa Kristo.

## KULIFUNDISHA SOMO

(Waulize wanafunzi kufungua vitabu vyao katika ukurasa wa



alimpa Filipo uwezo wa kuwaponya wagonjwa. Tokeo la mahubiri na miujiza ya Filipo ni kwamba Wasamaria wengi walimwamini Yesu kama Mwana wa Mungu aliye hai.

Kabla ya Filipo kuwasili Samaria, palikuwapo mtu mmoja aliyeitwa Simoni ambaye alikuwa akiwashangaza watu kwa uchawi wake. Je! umepata kumwona mtu akifanya uchawi? Sisi sote tunajua ya kuwa mambo ambayo wachawi hufanya ni hila tu za kutupumbaza sisi. Lakini Simoni hakuwafanya Wasamaria kujua kwamba matendo yake yalikuwa hila tu. Aliwafanya kufikiri kwamba yeye alikuwa mtu wa Mungu, na kwamba hila zake zilikuwa ishara za uwezo wa Mungu ndani yake.

Filipo aligundua mara moja ya kwamba Simoni alikuwa akiwadanganya watu. Na Wasamaria walipomsikia Filipo akihubiri habari za Kristo na wokovu, walimwacha Simoni, wakampokea Kristo. Simoni naye alipomsikia Filipo akihubiri habari za Kristo, alimwamini Kristo, akabatizwa. Lakini alikuwa bado anapendezwa na uwezo wa mitume wale kuliko vile alivyopendezwa na Bwana.

Baada ya siku chache, Petro na Yohana walikuja Samaria kumsaidia Filipo. Je! Simoni alijaribu kununua nini kutoka kwa mitume hawa? Kwa sababu Simoni alikuwa akiwadanganya watu kwa uchawi wake, labda alifikiri kwamba Petro na Yohana walijua hila fulani za siri ambazo yeye mwenyewe hakujua. Alitaka kuwapa pesa kama wangemwambia siri hiyo. Hakufahamu kwamba uwezo wa mitume wale ulikuwa kipawa cha Mungu.

Je! Petro alimkemea kwa jinsi gani? Alimwambia, "...Fedha yako na ipotelee mbali pamoja nawe, kwa kuwa umedhania ya kuwa karama ya Mungu yapatikana kwa mali." (Matendo 8:20)

Petro alikuwa akisema ya kwamba moyo wa Simoni haukuwa mnyofu mbele za Mungu. Alisema kwamba dhambi ya Simoni ilikuwa kama ukuta kati yake na Mungu. Simoni alijuta, akawasihi mitume wale kumwombea kwa Bwana asiadhibiwe.

Filipo alipomaliza kazi yake Samaria, Bwana alimtuma malaika wake kwake kumwambia, "Ondoka ukaende upande wa kusini hata njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda gaza." Je! malaika alimwambia Filipo sababu ya kwenda gaza? La.

Lakini Filipo ambaye alimweka Kristo kwanza maishani mwake, alitii mara moja. Kwa sababu wakati ule hapakuwa na motakaa, gari ya moshi au ndege, watu walisafiri kwa wanyama, kwa magari yaliyovutwa na wanyama (kama farasi au nyumbu), na kwa miguu. Labda Filipo alisafiri kwa miguu.

Je! ungekuwa tayari kutembea kilomita nyingi jangwani kama ungejua kwa hakika kwamba Mungu alikuwa anakuuliza kwenda huko? Jaribu kujifikiria mwenyewe kuwa

# KAZI YA FILIPO JANGWANI

**MASOMO YA BIBLIA: Matendo 8:1, 4-40**

## KUJIANDAA KUFUNDISHA

Katika somo hili utawafundisha wanafunzi wako habari za Filipo ambaye alipenda kumtii Mungu. Alikuwa na nia ya kwenda mahali po pote na kufanya jambo lo lote wakati Bwana alipomwambia "Nenda." Je! ni mara ngapi tunapofanya hivyo? Hata waalimu wa Shule ya Jumapili hufikiria kuwatembelea wanafunzi wao nyumbani, lakini sisi hujishughulisha zaidi na mambo yetu wenyewe na kukata shauri kwenda wakati mwingine. Labda Mungu anakwambia kwenda wakati ule unapojishughulisha na mambo yako mwenyewe.

Kusudi la somo hili ni kuonyesha kwamba Bwana alitumia Filipo kwa sababu Filipo alimtii. Pia, wewe kama mwalimu, unaweza kuwasaidia wanafunzi kukata shauri kumtii Bwana sikuzote.

## MAMBO YA KUKAZA

1. Bwana alitumia mateso kuwatawanya waamini wapate kumshuhudia katika mahali pengi mbali na Yerusalemu.

2. Filipo alipoamriwa na Roho Mtakatifu, aliondoka mara moja, akafuata uongozi wa Mungu mpaka kwa yule Mkushi.

3. Roho Mtakatifu huwaamuru waamini siku hizi katika kumtii Bwana.

## KULIFUNDISHA SOMO

Katika somo lililopita tulijifunza juu ya mtu wa kwanza kufa kwa ajili ya imani yake katika Kristo. Je! mtu huyo aliitwa nani? Ndiyo, aliitwa Stefano. Baada ya Stefano kuuawa, Sauli na marafiki zake walikwenda katika kila mji wakichoma mahali pa Wakristo pa mikutano na kuwafunga waamini gerezani. Wakristo wengi walikimbia kutoka Yerusalemu. Lakini walipotawanyika katika sehemu mbalimbali za ulimwengu, waliendelea kumshuhudia Kristo.

Filipo alikuwa akiwashuhudia watu wa mji wa Samaria. Huyu hakuwa mtume Filipo aliyesafiri pamoja na Yesu, bali alikuwa Myunani ambaye sasa alikuwa mwamini. Yeye, akiwa kama Stefano, alikuwa mmojawapo wa mashemasi wale saba waliochaguliwa na kanisa la Kikristo la Yerusalemu kusaidia katika kazi ya kuhudumu mezani.

Labda unaweza kukumbuka kusikia hadithi juu ya Msamaria mwema ya kwamba Wayahudi wengi waliwachukia Wasamaria. Lakini Filipo aliwaendea Wasamaria hao na kuwahubiria habari njema ya upendo wa Kristo. Alihubiri kwa uwezo mkuu, akidai ya kwamba Yesu ndiye aliyekuwa Masihi, yule anayewaokoa watu katika dhambi zao. Pia Mungu



kwanza. Waulize wanafunzi wasome mazungumzo yaliyotendeka katika hukumu ya Yesu. Mmoja anaweza kusoma maneno ya mahakama, na mwingine maneno ya Pilato, na kadhalika. Waeleze kwamba utawaambia wakati wa kusoma.)

Anza hivi: Baada ya Yesu kushikwa katika bustani, alipelekwa nyumbani kwa kuhani mkuu. Asubuhi yake, alipelekwa katika baraza la Wayahudi. Na Yesu aliposimama mbele ya baraza kadha watu walikuja mbele kumshtaki juu ya jambo fulani baya. Lakini hakuna hata mmoja wao aliyesema ukweli kuhusu Yesu. Hapakuwa na mtu wa kuwahoji mashahidi hawa. Hapakuwa na mtu aliyejitoa kusema ukweli kuhusu Yesu. Mwishowe, kuhani mkuu alisema: (Waambie wanafunzi wasome hukumu ya kwanza ya Yesu katika somo lao.)

Yesu aliposema kwamba alikuwa Mwana wa Mungu, kwa haraka yule kuhani mkuu na baraza lote walimshtaki kwa kusema jambo ambalo linamkufuru Mungu. Kulingana na sheria ya Kiyahudi, mtu ye yote ambaye alisema jambo linalomkufuru Mungu, ilikuwa lazima auawe. Lakini, kwa sababu Wayahudi walikuwa wameshindwa na kutawaliwa na serikali ya Kirumi, iliwabidi kutii sheria za Rumi. Moja kati ya sheria hizo ilikuwa kwamba, adhabu ya kifo iliweza kutolewa tu na mtawala wa serikali ya Kirumi. Kwa hivyo, walikata shauri kumpeleka kwa Pilato ambaye alikuwa liwali wa Rumi. Walijua kwamba Pilato hangefikiria jambo hili kuwa ni hatia, yaani, mtu kusema ati yeye ni Mwana wa Mungu. Pilato alikuwa Mrumi na pia hakumjua Mungu. Kwa hivyo, tutaona ya kwamba Wayahudi hawakumwambia Pilato kusudi lao hasa la kutaka Yesu ahukumiwe kifo. Badala yake, walijaribu kumfanya Pilato kuamini kwamba Yesu alikuwa mhalifu. Walimwambia uwongo kuhusu Yesu. (Wanafunzi wasome hukumu ya kwanza ya Yesu mbele ya Pilato.)

Uwongo walioutoa mara ya kwanza ulisemaje? (Kwamba Yesu aliwapotosha watu.) Walisema kwamba Yesu alikuwa akiwafanya watu wasiwe waaminifu kwa Mfalme wao wa Kirumi.

Uwongo walioutoa mara ya pili ulihusu nini? (Kwamba Yesu aliwaambia watu wasilipe kodi.)

Pilato alimwuliza Yesu, "Wewe ndiwe mfalme wa Wayahudi?" Yesu akajibu, "Wewe wasema." Pilato hakufahamu maana ya maneno haya, lakini aliona hakika ya kwamba Yesu hakustahili kuuawa.

Viongozi wa Kiyahudi walikasirika wakati Pilato alipotoa hukumu yake. Basi, wakaja tena na mashtaka mengine ya uwongo; ati; "Huwataharakisha watu, akifundisha katika Uyahudi wote, tokea Galilaya mpaka huku."

Pilato aliposikia kwamba Yesu anatoka Galilaya, alikusudia kumpeleka Yesu kwa mtawala wa Galilaya. Mtawala huyo alikuwa Herode, aliyekuwa kwa wakati huu akitembelea Yerusalemu. Babu yake,

yaani Mfalme Herode, ndiye aliyejaribu kumwua Yesu wakati alipozaliwa Bethlehemu. Pilato alifurahi kuepukana na shida hii kubwa, kwa hivyo alimpeleka Yesu kwa Herode.

Kwa muda mrefu Herode alikuwa akitaka sana kumwona Yesu. Alitaka kumwona Yesu akifanya mwujiza. Lakini Yesu hakuridhisha upekuzi (au tamaa) wa mtu huyu mwovu. Hata alikataa kuzungumza na Herode. Hakujibu hata swali moja.

Herode aliudhika, lakini akakata shauri kwamba ni lazima amdhihaki Yesu. Akisaidiwa na askari wake walimvisha Yesu mavazi kama kumfanya mfalme. Herode akamdhihaki kisha akamrudisha kwa Pilato.

Kwa mara nyingine Pilato alimhoji Yesu, akakata shauri kwamba Yesu hakuwa na hatia. Kisha aliwaita viongozi wa dini, akawaambia kwamba Yeye na Herode walikata shauri kwamba Yesu hakustahili kufa. (Wanafunzi wasome hukumu ya pili ya Yesu mbele ya Pilato.)

Kila mwaka, wakati wa karamu ya Pasaka, liwali alimfungua mfungwa mmoja ye yote ambaye watu walimpendelea. Pilato alifikiri kwamba kama watu hawa wangekumbushwa desturi hii, wangemchagua Yesu afunguliwe kuwa huru. Lakini, mara tu Pilato alipotoa wazo hili, watu walipaza sauti zao wakisema, "Msulibishe Yesu. Tufungulie Baraba."

Baraba alikuwa amefungwa gerezani kwa sababu alikuwa mwizi na mwuaji na pia alikuwa ameongoza kikundi fulani kuipindua serikali. Watu walikuwa tayari kumwacha mwuaji huyu aishi kama wangeruhusiwa kumwua Yesu.

Pilato alijaribu kujadiliana na kundi lile, lakini waliendelea kusema kwamba Yesu asulibiwe. Pilato aliiosha mikono yake na maji kwa kujaribu kuonyesha kwamba hakuwa na hatia katika kifo cha Yesu. Aliwaambia kwamba wakitaka wamchukue Yesu wakamsulibishe. Wayahudi walijibu pamoja, wakisema, "Damu yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu." (Mathayo 27:25) Walikuwa tayari kuzichukua lawama zote.



Pilato alipowafungulia Baraba, Wayahudi walimkabidhi Yesu mikononi mwa askari wa Kirumi



kubadilishwa. Alieleza kwamba, Mungu, kwa (Mwanawe Yesu) ~~(Nabii Isaya)~~, alikuwa ametoa mambo mema zaidi kuliko hekalu na torati.

Tunasoma katika Matendo 7:57-59 ya kwamba watu wa baraza walimkasirikia sana Stefano, wakamburuta na kumtoa nje ya mji. Huko walimpiga kwa mawe mpaka akafa. Watu wale waliompiga kwa mawe walivua nguo zao wakaweka miguuni pa kijana mmoja aliyezitunza. Andika jina la kijana huyo.___SAULI___

Andika maneno ya mwisho ya Stefano aliyoyasema kabla ya kufa.

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

**KIFUNGU CHA KUKUMBUKA**

**"Lo lote mkono wako utakalolipata kulifanya, ulifanye kwa nguvu zako."**
**Mhubiri 5:10a**

**WAKATI WA KUFUNGA**

Stefano ameheshimiwa kwa karne nyingi kama mfia dini wa kwanza wa kanisa la Kikristo. Tunasifu ushujaa wake na uaminifu kwa Kristo wakati alipokabiliwa na hukumu ya kufa. Lakini Stefano hakuwa shujaa mara moja. Wakati alipokuwa akiishi, alijitoa kwa Yesu. Alimweka Kristo kwanza maishani mwake kila siku akijaribu kujua mambo ambayo Kristo alimtaka kufanya, na kufanya mambo hayo kwa furaha na bidii.

Labda unafikiri kwamba siku moja, baada ya wewe kuwa mtu mkubwa ndipo utakuwa shujaa wa Kristo. Labda unaweza kufikiria ati unaweza kubadilika mara moja kwa kuacha kufanya mambo madogo uliyokuwa ukimfanyia Kristo na kuwa Mkristo mpevu. Hii haiwezekani kamwe. Ni muhimu kukua kiroho kama unavyokua kimwili. Kukua kimwili kunahitaji chakula, maji, mazoezi, mapumziko na mambo mengine. Lakini kukua kiroho kunahitaji maombi, kusoma Biblia na kujifunza, kutii amri za Yesu na kuwatendea wengine mambo mema na ndiyo utakapoweza kuwa Mkristo mpevu. Je! ni lini ambapo utaanza hivyo? Sasa hivi! Utakapokwenda nyumbani leo, fikiri, "Je! naweza kufanya nini ili nianze kujifunza na kujiendeleza kuwa Mkristo shujaa?" Kumbuka kifungu cha kukumbuka cha leo.

**KAZI YA KUFANYA**

Katika kanisa la kwanza, waamini wote walishiriki pamoja chakula na vitu vingine. Waamini wengine walikuwa wanawake ambao mabwana wao walikuwa wamekufa (yaani, wajane). Soma Matendo 6:1-4 upate kuona mojawapo ya shida ambazo wanawake hao walikuwa nazo. Kisha, kata maneno yasiyo kweli katika sentensi hizo hapo chini.

Wakristo wa Kiyunani walinung'unika kwamba wajane wao ~~(walilishwa kupita kiasi)~~ (walisahauliwa) katika huduma ya kila siku.

Mitume wale kumi na wawili waliona kwamba haikuwapasa kuacha kufundisha Neno la Mungu la kuhudumu mezani. Kwa hivyo, waliwaambia washiriki wa kanisa kuwachagua watu ~~(wanane)~~ (saba) wema, wanyenyekevu na wanaomcha Mungu kutumikia mezani.

Kisha mitume wangeweza kutumia wakati wao mwingi ~~(kuandika)~~ (katika kuomba) na kufundisha Neno la Mungu.

Mara kwa mara mtu anapoishi kwa njia ya kumpendeza Mungu, watu ambao hawampendi Mungu huwa maadui wake. Soma katika Matendo 6:9-12 habari kuhusu mambo yaliyomfanya Stefano kuhukumiwa. Kisha andika namba (1) kando ya jambo lililofanyika kwanza, na namba (2) kando ya lile lililofuatia. Fanya hivyo mpaka mambo hayo yote yamalizike.

**_2_ Maadui wa Stefano hawakuweza kushindana naye kwa sababu ya hekima yake.**

**_1_ Watu walishindana na Stefano juu ya Yesu.**

**_4_ Walitaharakisha watu, wakamkamata Stefano.**

**_5_ Walimleta Stefano mbele ya baraza.**

**_3_ Waliwaajiri watu waliosema uongo kwamba Stefano aliwakufuru Musa na Mungu.**

**Soma juu ya sehemu ya kwanza ya hukumu ya Stefano mbele ya baraza la Wayahudi katika Matendo 6:13-15. Wakati unapokata majibu yasiyo kweli, fikiri juu ya hukumu hiyo. Je! unafikiri ilikuwa hukumu ya haki?**

1. Maadui wa Stefano walisimamisha mashahidi wa ~~(kweli)~~ (uwongo) waliosema, "Mtu huyu haachi kusema maneno ya kufuru juu ya mahali hapa (patakatifu) ~~(pazuri)~~ na juu ya torati. Maana tumemsikia akisema kwamba (Yesu) ~~(Petro)~~ atapaharibu mahali hapa, na kuzibadili desturi tulizopewa na ~~(Herode)~~ (Musa)."

2. Watu wote walioketi katika baraza walimkazia Stefano macho yao. Walimwona ~~(mwili mzima)~~ (uso) wake kuwa kama uso wa (malaika) ~~(kiongozi)~~.

3. Baada ya watu wale kumshuhudia uwongo, Stefano alijaribu kuonyesha (baraza) ~~(mitume)~~ hakuwa akilaumu wakati aliposema hekalu lingeharibiwa na torati ya (Musa) ~~(Ibrahimu)~~



ambao kazi yao ilikuwa ni kuwasulibisha wafungwa. Mtu ye yote aliyehukumiwa kusulibiwa, ilimbidi kuubeba msalaba wake yeye mwenyewe. Lakini Yesu alikuwa mdhaifu. Kwa muda mrefu alikuwa amekaa bila chakula na usingizi. Walikuwa wamempiga. Haya yote yalimfanya kutoweza kuubeba msalaba wake peke yake. Makutano wale walipoondoka mle mjini, walikutana na mtu mmoja aliyeitwa Simoni, Mwafrika. Askari wa Kirumi walimlazimisha kumsaidia Yesu kuubeba msalaba wake.

Makutano ya watu wale walikwenda mpaka mahali palipoitwa Fuvu la Kichwa. Katika mahali hapo ndipo marafiki wa Yesu waliokuwa na huzuni nyingi walimwangalia akipigiliwa misumari ya miguu na mikono juu ya msalaba. Kisha waliinua msalaba na kuuweka kwenye shimo ambalo walikuwa wamelichimba kwa kusudi hilo. Juu ya msalaba Pilato aliwaamuru askari waweke anwani yenye maneno yaliyoandikwa katika lugha tatu, Kiyunani, Kirumi na Kiebrania. Maneno haya yalisema, "Huyu ndiye Mfalme wa Wayahudi."

Je, wawakumbuka wale waliosulibiwa pamoja ya Yesu? Ndiyo, walikuwa wanyang'anyi wawili. Yesu, Mwana wa Mungu, alitundikwa msalabani pamoja na wahalifu wawili, kana kwamba alikuwa mmoja wa wahalifu wale. Mmoja wa wahalifu wale alimwambia Yesu, "Ikiwa wewe ni Kristo, jiokoe nafsi yako na sisi." Lakini mhalifu wa pili akamjibu, akisema, "Wewe humwogopi hata Mungu, nawe u katika hukumu iyo hiyo? Nayo ni haki kwetu sisi, kwa kuwa tunapokea malipo tuliyostahili kwa matendo yetu, bali huyu hakutenda lo lote lisilofaa." Kisha akasema, "Ee Yesu, nikumbuke utakapoingia katika ufalme wako."

Je, Yesu alimjibu nini? "Amini, nakuambia, leo hivi utakuwa pamoja nami peponi." (Luka 23:43)

Ilikuwa yapata saa tatu, ndipo Yesu alipoangikwa msalabani. Ilipotimia saa sita, kukawa giza juu ya nchi yote. Kwa masaa matatu jua lilipungua nuru yake. Ilikuwa yapata kama saa tisa hivi, ndipo Yesu alilia kwa sauti kuu, akasema, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?" (Mathayo 27:45)

Mungu alikuwa amemwacha Yesu! Kwa nini? Kwa sababu Yesu alizichukua dhambi za watu wote ambao waliishi na ambao wataishi, pamoja na wewe na mimi, kama kwamba alikuwa ametenda makosa.

Mwishowe kazi ya Yesu ya kuteseka kwa ajili ya dhambi za ulimwengu ilimalizika. Kwa sauti kuu, akasema, "Ee Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu." Watu waliotazama kwa mbali waliingiwa na woga na huzuni. Mmoja wa askari wa Kirumi alisema, "Hakika mtu huyu alikuwa Mwana wa Mungu." (Mathayo 27:54)

Mmoja kati ya marafiki wa Yesu waliokuwa pale alikuwa mtu tajiri aliyeitwa Yusufu wa Arimathaya. Yusufu alikuwa mmoja kati ya wale wanachama wa Baraza la Kiyahudi.

Yeye pamoja na wengine hawakukubaliana na wenzao kumhukumu Yesu kufa. Ingawa kabla ya hayo alikuwa mfuasi wa Yesu wa siri, sasa alipata ujasiri wa kumwendea Pilato kuutaka mwili wa Yesu. Alikuwa na kaburi lake mwenyewe ambalo lilikuwa limechongwa mwambani. Lilikuwa bado halijalazwa maiti yo yote ndani. Alishusha mwili wa Yesu msalabani, akaufunga kwa sanda na kuuweka kaburini. Kisha jiwe lilivingirishwa kwenye mlango wa kaburi.

Wale wanawake waliokuja na Yesu toka Galilaya, walimfuata Yusufu kuona mahali ambapo angeuzika mwili wa Yesu. Kisha wakarudi nyumbani kutayarisha manukato na marhamu. Haya yalikuwa ni kuongezea yale ambayo Yusufu alikuwa amekwisha kuweka kwa mwili wa Yesu.

**KAZI YA KUFANYA**

Majibu mawili yametolewa kwa kila swali hapo chini. Ni jibu moja tu ndilo sawa. Piga mstari chini ya jibu hilo lililo sawa.

1. Baraza la Wayahudi walipomwuliza Yesu ikiwa yeye alikuwa Mwana wa Mungu, Yesu alijibu, "Ndimi." Kweli au Si kweli?

2. Yesu alihukumiwa mara ngapi? Mara tatu au mara nne?

3. Pilato alifikiri kuwa Yesu alikuwa na hatia na akakubaliana na Wayahudi kwamba ilimpasa Yesu kufa. Kweli au Si kweli?

4. Herode alifurahi kuwa na nafasi ya kukutana na Yesu kwa sababu (alimtaka aseme mithali) (alimtaka afanye miujiza).

5. Mfungwa ambaye alifunguliwa alikuwa (Yusufu wa Arimathaya) (Baraba).

6. Maandishi yaliyokuwa msalabani yalisema, "Huyu ndiye Mfalme wa Wayahudi." Kweli au Si kweli?

7. Ni wahalifu wangapi waliosulibiwa pamoja na Yesu? Wawili au Watatu?

Soma Luka 23:44-46. Kamilisha sentensi zilizoko chini ya picha. Sentensi zilizokamilishwa zitaeleza jambo ambalo kila mtu katika picha hiyo alifanya baada ya kufa kwake Yesu.



Akida alimtukuza Mungu (Luka 23:47)



alifufuka katika wafu baada ya wao kumwua. Ingawa hawakutaka kuamini, walijua mambo mengi ya ajabu yaliyofanyika wakati Yesu alipokufa. Pia, walijua kazi ya Petro na Yohana na miujiza waliyokuwa wakifanya kwa jina la Yesu.

Halafu Stefano alitazama mbinguni. Je! unaweza kuona kitu cho chote kilicho ndani ya mbingu? La, lakini Stefano aliona. Ulikuwa mwujiza. Bwana alimwezesha Stefano kuona utukufu wake na Yesu alikuwa amesimama mkono wa kuume wa Mungu. Mungu alikuwa akimwonyesha Stefano kwamba yeye hawaachi wanafunzi wake peke yao hata wakati wa kufa.

Stefano alipowaambia watu wa baraza kwamba anaona maono, walianza kupiga kelele na kuziba masikio yao. Kisha waliondoka katika chumba kile cha baraza, wakamkamata, wakamburuta mkapa nje ya kuta za mji. Walipokuwa wamekwisha kumtoa nje ya mji wao "mtakatifu", walianza kumpiga kwa mawe.

Ingawa Stefano alisikia uchungu mwingi kila wakati ambapo jiwe lilipompiga, aliendelea kuomba. Alimwomba Yesu kupokea roho yake. Alipojua ya kwamba baada ya muda mfupi angekufa, alikuwa na tamaa ya roho yake kwenda kukaa pamoja na Yesu.

Kabla ya kufa, Stefano alipiga magoti akalia kwa sauti kuu, "Bwana, usiwahesabie dhambi hii!" Baada ya kuwasamehe wale waliokuwa wakimwua, kama Yesu alivyofanya, Stefano alikata roho.

Watu wale waliompiga Stefano kwa mawe walikuwa wamevua nguo zao na kuweka miguuni pa kijana mmoja rafiki yao, aliyeitwa Sauli. Itatupasa kumkumbuka Sauli kwa maana tutajifunza habari zake katika masomo mengine yajayo.



Mungu na Musa. Na kwa njia hii waliwataharakisha watu.

Kisha kundi la watu wenye hasira walikusanyika wakamkamata Stefano wakampeleka mbele ya baraza ambalo ndilo lililokuwa mahakama kuu ya Wayahudi.

Mashahidi wa uwongo waliwaambia baraza, "Mtu huyu haachi kusema maneno ya kufuru juu ya mahali hapa patakatifu na juu ya torati; maana tumesikia akisema kwamba Yesu huyo Mnazareti atapaharibu mahali hapa, na kuzibadili desturi tulizopewa na Musa." Matendo 6:13b-14).

Watu wote walioketi katika baraza walimkazia Stefano macho. Uso wake ulionekana kuwa kama uso wa malaika! Alikuwa mpole, mtulivu, na mwenye amani.

Hukumu ya Stefano iliendelea. Kuhani mkuu alimwuliza Stefano kama mambo haya yalikuwa kweli. Badala ya kujibu "ndiyo" au "la," Stefano alitumia nafasi hii kuwaambia Wayahudi wale habari za Yesu, Mwana wa Mungu. Alisema kwa ushujaa bila kuwa na wasiwasi juu ya matokeo ya hukumu yake.

Watu wale walimshtaki Stefano kwa kusema maneno ya kupinga hekalu. Stefano aliwaonyeshá katika historia yao wenyewe ya kwamba hakuna mahali po pote pa ibada ambapo ni patakatifu zaidi kwa Mungu kuliko mahali pengine.

"Ndugu zangu na dada zangu, sikilizeni," alisema. "Mnajivunia babu zetu; Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Yusufu, Musa, Yoshua, na Daudi. Mungu alisema na watu hawa wote wakuu, akiwapa ahadi zake takatifu. Lakini hakuna hata mmoja kati yao aliyeabudu ndani ya hekalu."

Stefano aliendelea kueleza kwamba sikukuu zao zote katika hekalu lao njema zilipangwa na Mungu ili kutayarisha mioyo ya watu wake kumpokea Yesu Kristo, Masihi aliyeahidiwa kuja. Kwa sababu Kristo alikuwa amekwisha kuja, sheria za zamani na sikukuu hazikuhitajika tena.

Mungu hahitaji nyumba iliyojengwa kwa mkono wa mwanadamu. Basi hayupo tu hekaluni au kanisani. Hakuna jengo lililo kubwa zaidi kumtosha Mungu. Sisi hujenga makanisa kwa kusudi la kumwabudu Mungu ndani yao, lakini Mungu anaweza kusema nasi mahali po pote.

Kisha, Stefano alibadili mambo. Alianza kuwahukumu watu wa baraza. Aliwaonyesha jinsi kwa karne nyingi watu wa Israeli wamekuwa wakimkataa Bwana. Watu wa baraza walikasirika, na kuzidi kukasirika sana alipowaambia, "Babu zenu waliwaua manabii waliotabiri kuja kwa yule Mwenye Haki (Yesu), na sasa mmemsaliti na kumwua, ninyi mliopokea torati kwa agizo la malaika msiishike."

Watu wa baraza hawakukasirika tu, bali pia walichomwa mioyo kwa sababu walijua kulikuwa na ukweli katika maneno ya Stefano. Stefano alidai ya kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, na kwamba





Makutano yote walijipigapiga <u>vifua</u> (Luka 23:48)



Wanawake wakasimama kwa <u>mbali.</u> (Luka 23:49)

**KIFUNGU CHA KUKUMBUKA**

**"Yesu alijitoa nafsi yake kwa ajili ya dhambi zetu, ili atuokoe na dunia hii mbovu iliyopo sasa." Wagalatia 1:4**

**WAKATI WA KUFUNGA**

(Waulize wanafunzi wafikirie kuhusu maswali yafuatayo. Yasome maswali, lakini usingojee majibu yake.)

Kwa nini Yesu aliwaruhusu askari wa Kirumi wamipigilie misumari msalabani?

Kwa nini aliwaruhusu makutano ya watu kumdhihaki wakati alipokuwa akiteseka?

Je, angeweza kujiokoa wakati ule wa dakika ya mwisho?

(Sema:) Mwana wa Mungu, Yesu, alikuwa na uwezo wa kujiokoa mwenyewe, lakini badala ya kujiokoa, alijitoa mwenyewe, hasa aliyatoa maisha yake kwa ajili yetu. Kwa nini?

Tukiseme tena pamoja kifungu chetu cha kukumbuka.

Ni kwa ajili ya dhambi za nani zilizomfanya Yesu kujitoa mwenyewe msalabani? (Kwa ajili ya dhambi zako na zangu.) Yesu akutaka umtegemee yeye ili upate furaha ya kuwa kwa ukamilifu katika mapenzi ya Mungu.

Funga kwa maombi ili kwamba Mungu atusaidie kuishi kila siku katika mapenzi yake, na kumshukuru Mungu kwa kifo cha Yesu ambacho hutupa maisha ya milele.

# YESU AFUFUKA KATIKA WAFU

**MASOMO YA BIBLIA: Luka 24:1-49**

**KUJIANDAA KUFUNDISHA:**

Kusudi la somo hili ni kuwasaidia wanafunzi kujua kwamba Yesu ni Mwokozi wetu anayeishi milele. Tunaweza kujua msamaha wa dhambi zetu kwa sababu Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu. Lakini, kuna mambo mengi zaidi yanayohusu kifo cha Yesu. Pia, alifufuka tena! Na kwa sababu alifufuka tena anaweza kuwa bwana wetu sasa tunapoishi, na Bwana wetu katika wakati ujao tutakapokufa. Kusudi la Mungu kutuokoa ni kwamba Mwanawe atatutawala kama Bwana wa kila sehemu ya maisha yetu. Kutambua kwamba Yesu alifufuka katika wafu peke yake, hakutoshi. Ni lazima tutambue ya kwamba mwokozi wetu Kristo, anastahili na kuhitaji nafasi ya kwanza katika maisha yetu. Yesu anataka tumfanye kuwa Bwana wetu! Je! Kristo, kwa kweli ni Bwana wa kila sehemu ya maisha yako?

**MAMBO YA KUKAZA**

1. Marafiki wa Yesu hawakumtumainia yeye kufufuka tena.

2. Kifo cha Yesu, kuzikwa kwake, na ufufuo wake, yalitokea kama yalivyosemwa hapo mbeleni na mafundisho ya Agano la Kale.

3. Na kwa sababu Yesu alifufuka katika wafu, anatoa maisha yake kwa kila mmoja anayeamini kwake.

4. Yesu ni Mwokozi wetu anayeishi milele, na anahitaji kuwa bwana wa maisha yetu.

**KULIFUNDISHA SOMO**

Kuna nyimbo nyingi nzuri za kuimba wakati wa Pasaka. Unaweza kufikiria nyingine, lakini uweke pia ule usemao, "Mle Kaburini."

(Sema:) Tunaadhimisha sikukuu ya Krismasi kila mwaka. Siku hiyo ni yenye maana sana kwa sababu ndiyo siku tunayokumbuka tukiwa na maajabu mioyoni mwetu juu ya kuja kwa Mwana wa Mungu kama mtoto mchanga. Je! hiyo pekee inatosha? Ni kwa sababu gani tunaadhimisha Pasaka? Maana yake ni nini? (Ngoja kidogo ili upate majibu. Kisha uliza maswali mengine yanayofuata bila kutoa muda wa kuyajibu. Maswali haya ni ya kuwafanya wanafunzi kufikiri.)

Je! ufufuo wa Yesu ni wa maana? Kufuka kwake katika wafu kuna maana gani kwetu sisi wakati huu? Hebu tuangalie jambo lililotendeka Yerusalemu miaka 2,000 iliyopita ili tupate majibu ya maswali haya.

Wakati Yusufu wa Arimathaya aliposhusha mwili wa Yesu msalabani, wanawake wengine walimfuata ili kuona mahali ambapo angemzika Yesu. Walimwangalia Yusufu akiulaza mwili wa Yesu ndani ya kaburi. Kisha wakarudi kwao



kwa sababu ya imani yao. Waamini walishinda hii kwa upendo. Wale waliokuwa na pesa waliwalinda wale ambao hawakuwa nazo. Jambo hili lilileta shida nyingine. Baadhi ya Wakristo wale waliokuwa Wayahudi waliokaa katika nchi nyingine. Walizungumza lugha mbalimbali na kuvaa mavazi tofauti. Walianza kunung'unika kwamba watu wao maskini hawakupata usaidizi wa kutosha kama wale waliokaa Uyahudi (Palestine). Manung'uniko haya yaliendelea yakawa ugomvi. Jambo fulani lilipasa kufanywa kumaliza ugomvi huo.

Petro aliwaita watu wote pamoja. Watu saba wakachaguliwa kufanya kazi ya kuwatunza maskini wale. Hebu tazama kwamba watu hao saba walipaswa kuwa wa namna gani. Ingawa hawakuwa wachungaji au wâhubiri, iliwapasa kuwa waaminifu. Tunaweza kuona sababu ya jambo hili. Wangepewa wajibu wa kusimamia pesa. Walipaswa kuwa watu wema waliojawa na hekima. Wangehitaji hekima kukata shauri kwamba ni nani aliyehitaji msaada au ni nani ambaye alikuwa mzembe na mwenye choyo. Walipaswa kujawa na Roho Mtakatifu. Kwa mambo haya, tunajifunza kwamba tunahitaji kujawa na Roho Mtakatifu, sio tu kwa kazi ya uchungaji bali kuwa wanafunzi waaminifu, marafiki wa kweli na wenye hekima, na Wakristo waaminifu. Kila kitu ambacho Mkristo hufanya, kinapaswa kuongozwa na Roho Mtakatifu.

Mtu wa kwanza kuchaguliwa alikuwa Stefano. Stefano anazungumzwa habari zake kama mtu "aliyejaa imani na Roho Mtakatifu." Ingawa kazi yake ilikuwa ni kutumikia mezani, hakufanya kazi hiyo tu. Alikuwa amejitoa kwa Bwana. Kwa hivyo, alitafuta njia nyingine za kumtumikia Mungu. Alitaka kuonyesha maisha yake kwamba alimpenda Bwana. Labda Stefano alijua maneno ya Agano la Kale ambayo tunataka kuyakumbuka leo. Yanatoka katika kitabu cha Mhubiri 9:10. "Lo lote mkono wako utakalolipata kulifanya, ulifanye kwa nguvu zako."

Katika wakati wa historia, hekalu na masinagogi yalitumiwa kama Shule za vijana wa Kiyahudi. Baada ya Yesu kupaa juu mbinguni, wanafunzi wake walikuwa waaminifu kuhubiri Injili katika masinagogi haya. Kwa muda mfupi waalimu wengine walianza kuona wasiwasi juu ya wanafunzi wa Yesu kupendwa na watu wengi. Walisema kukua na kuongezeka kwa Wakristo kuliwafanya watu wachache sana kuamini njia za zamani. Waalimu hawa waliamini kwamba njia za zamani za kuabudu ndizo zilizokuwa njia za kweli za kumwabudu Mungu. Kwa hivyo, viongozi wa Kiyahudi, mara kwa mara walipingana na Wakristo. Lakini wakati walipoanza kupingana na Stefano, walijiona kuwa hawangeweza kumshinda kwa sababu Stefano alipokea majibu yake kutoka kwa Mungu. Hawakuweza kushindana na hekima yake, kwa hivyo waliwashawishi watu waliosema uwongo juu yake. Walieneza uwongo ya kwamba Stefano aliwatukana

# SHAHIDI ALIYEKUFA KWA AJILI YA KRISTO

**MASOMO YA BIBLIA: Matendo 6:1 - 7:60**

## KUJIANDAA KUFUNDISHA

Vijana hupenda kujifikiria wenyewe kuwa katika hali ngumu. Hii ni vizuri na wewe kama mwalimu unaweza kuwasaidia kujaribu kufikiri kama Stefano alivyofikiri. Wasaidie kujua kwamba wanaweza kuwa kama Stefano sasa kwa kumweka Kristo kwanza maishani mwao. Stefano hakuwa shahidi mkubwa wa Kristo wakati siku ile tu alipokufa. Alikwisha kuwa ushuhuda wa upendo wa Kristo kwa siku nyingi sana kwa kumpa Kristo nafasi ya kwanza maishani mwake kila siku.

Kusudi la mafundisho yako linaweza kuwa kuonyesha kwamba Stefano alimweka Kristo kwanza katika mambo aliyofanya na kusema. Pia, waonyeshe wanafunzi kwamba inawapasa kumweka Kristo kwanza maishani mwao na kumtumikia mahali po pote walipo.

## MAMBO YA KUKAZA

1. Kwa sababu Stefano alimweka Kristo kwanza maishani mwake, aliweka moyo wake katika kila jambo alilofanya, hata kama ilikuwa kuhudumu mezani au kushuhudia.

2. Stefano alithibitisha kwa kifo chake kwamba alikuwa shujaa wa Bwana.

3. Hatuwi Wakristo mashujaa kwa ghafula; bali tunakuwa pole pole na kumweka Kristo kwanza katika maisha yetu ya kila siku.

## KULIFUNDISHA SOMO

Anza kusema: Je! ndugu yako mdogo angeweza kukimbia mbio na Kipchoge Keino kesho? La. Kwanza ni lazima kufanyika nini? Ni lazima akue na kuwa kijana mwenye nguvu. Lazima ajifunze sheria za kukimbia. Lazima afanye mazoezi ya mbio kwa miaka mingi sana kabla ya kuwa mkimbiaji hodari."

Je! inawezekana kwa Mkristo "kutokuwa hodari" katika mambo ya kiroho? Ikiwa hufanyi mazoezi ya kuwa Mkristo, hutaweza kuwa mtu shujaa wa Mungu mara moja. Lazima tuishi maisha yetu kila siku kwa kufuata mfano wa Yesu.

Andika karatasini: "JE! NI LINI NINAPOWEZA KUWA MKRISTO SHUJAA?"

Somo hili ni juu ya Stefano. Je! alikuwa Mkristo shujaa? Ni lini alipokuwa shujaa? Utakapoweza kujibu swali hili la mwisho, pia utajua jibu la swali lile lililoandikwa karatasini.

Kanisa lilipokuwa na kuongezeka shida zake pia ziliongezeka. Mojawapo ni kwamba maskini wengi walimwamini Yesu wakajiunga na kanisa. Labda wengine kati yao walipoteza nyumba zao au kazi zao



kuandaa manukato na marhamu kuja kuupaka mwili wa Yesu kama ilivyokuwa desturi siku hizo.

Na kwa sababu siku ya pili ilikuwa Sabato ya Wayahudi (Jumamosi) na hakuna mtu ye yote aliyeruhusiwa kufanya kazi yo yote siku hiyo, wanawake wale walikaa nyumbani kwao. Kisha, siku ya kwanza ya juma (Jumapili), waliamka mapema na kuchukua manukato na marhamu yao, wakaenda kaburini.

Walipokuwa wakienda, walikuwa na wasiwasi njiani jinsi wangeweza kulisukuma lile jiwe kubwa mlangoni pa kaburi. Walipofikia kaburi, waliona ya kuwa lile jiwe limevingirishwa. Walifurahi kuona kwamba shida yao imetimizwa, wakaingia ndani ya kaburi. Lakini walikuta kama mwili wa Yesu ulikuwa hauko pale.

Je, ni jambo gani hili ambalo lilitukia? Wanawake wale walipokuwa wakisimama ndani ya kaburi lile, wakifikiria jambo la kufanya, kwa ghafula waliwaona malaika wawili. Wakainamisha nyuso zao chini; wakiwa katika hali ya hofu.

Kisha walisikia malaika wale wakiwaambia, "Kwa nini mnatafuta aliye hai katika wafu? Hayupo hapa, amefufuka. Kumbukeni alivyosema nanyi alipokuwa angaliko Galilaya, akisema Imempasa Mwana wa Adamu kutiwa mikononi mwa wenye dhambi, na kusulibiwa, na kufufuka siku ya tatu." (Luka 24:5b, 6, 7)

Mara ile wanawake wale wakakumbuka mambo ambayo Yesu aliwaambia. Kwa hivyo, lile kaburi lililokuwa tupu, na malaika wale walithibitisha kwamba maneno ya Yesu yalitimia! Wanawake wale walirudi upesi kuwaambia wafuasi wa Yesu habari hii yao ya furaha!

Habari hii ya wanawake hawa ilionekana kwa mitume kuwa kama hadithi isiyo ya kweli, kwa hivyo hawakuweza kuiamini. Lakini Yohana na Petro walikata shauri kwenda kaburini kujionea wenyewe jambo lililotendeka. (Yohana 20:3-10). Walikimbia kwenda kaburini, wakaingia na kuangalia ndani. Walishangaa! Waliviona vitambaa vya sanda vimelala lakini mwili wa Yesu ulikuwa hauko. Nguo za mazishi (sanda) ambazo zilitumiwa wakati ule zilikuwa vipande virefu vilivyozongwazongwa maiti. Na katikati ya kunjo paliwekwa ratili nyingi ya manukato na marhamu. Ilikuwa desturi ya Wayahudi kutumia nguo nyingine kufungia kichwa cha maiti.

Lazaro alipotoka kaburini, Bwana aliwaambia watu kumfungua na kuondoa zile nguo alizofungwa nazo (Yohana 11:44). Lakini katika kaburi la Yesu sanda ilikuwa bado ingali pale ambapo Yesu alilazwa jinsi ilivyokuwa imefungwa. Kile kipande cha kufungia kichwa kilikuwa mahali pa peke yake na Yesu alikuwa ameondoka! Haiwezekani mwili kuondolewa katika sanda aliyofungwa nayo na sanda ile ibaki kama ilivyokuwa. Ni lazima sanda ile ifunguliwe au kupasuliwa. Lakini Petro na Yohana waliona vipande vile vikiwa jinsi vilivyofungwa, lakini mwili

haukuwako. Walistaajabia maana yake.

Kuna neno kuhusu jambo ambalo Yohana na Petro walifanya ambalo linaweza kuwa onyo kwetu. Watu hawa wawili waliona thibitisho la ufufuo walakini jambo walilofanya lilikuwa ni kwenda nyumbani tu.

Mariamu hakwenda nyumbani na twasoma katika kitabu cha Yohana kwamba Yesu alikuja na kusema naye. (Yohana 20:11-18)

Adhuhuri ile, Kleopa na rafikiye, walikuwa wakitembea kutoka Yerusalemu kwenda Emau, kijiji kidogo ambacho ni kama maili saba hivi kutoka mjini. Walipokuwa wakitembea, walikuwa wakizungumza wao kwa wao juu ya mambo yaliyotendeka siku tatu zilizopita. Wakati wa asubuhi ile tundipo waliposikia habari mpya kwa wanawake wale ya kuwa kaburi la Yesu lilikuwa tupu.

Na walipokuwa wakizungumza, Yesu alikaribia na kuandamana nao. Lakini hawakumtambua. Yesu aliwauliza jambo walilokuwa wakizungumza. Kleopa akamwuliza, "Je! wewe peke yako u mgeni katika Yerusalemu, hata huyajui yaliyotukia humo siku hizi?" (Luka 24:18)

Yesu akawauliza, "Mambo gani?"

Wakamjibu, "Mambo ya Yesu wa Nazareti aliyekuwa mtu nabii, mwenye uwezo katika kutenda na kunena mbele za Mungu na watu wote; tena jinsi wakuu wa makuhani na wakubwa wetu walivyomtia katika hukumu ya kufa, wakamsulibisha. Nasi tulikuwa tukitumaini ya kuwa yeye ndiye atakayewakomboa Israeli. Zaidi ya hayo yote, leo ni siku ya tatu tangu yalipotendeka mambo hayo." Luka 24:18-21)

Waliendelea, "Tena wanawake kadha wa kadha wa kwetu walitushitusha, walipokwenda kaburini asubuhi na mapema, wasione mwili wake; wakaja wakasema ya kwamba wametokewa na malaika waliosema kwamba yu hai. Na wengine waliokuwa pamoja nasi walikwenda kaburini wakaona vivyo hivyo kama wale wanawake walivyosema, ila yeye hawakumwona." (Luka 24:22-24)

Yesu alianza kuwafundisha. "Akawaambia Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyoyasema manabii! Je! haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia utukufu wake?" (Luka 24:25-26)

Kisha Yesu akaeleza sehemu nyingine za maandiko ya Agano la Kale ambayo yameandikwa juu yake, akianzia na vitabu vya Musa (Sheria) na Maandiko ya manabii.

Yesu na watu wale wawili walipokaribia Emau, kijiji ambacho Kleopa na rafiki yake walikuwa wakienda kukaa, walimwomba kukaa nao usiku ule.

Walipokaa kula chakula chao cha usiku, Yesu aliutwaa mkate, akaubariki, akaumega, akawapa. Kwa ghafula macho yao yalifumbuliwa, wakamtambua.



kuhani mkuu aliwauliza mitume, na jinsi mitume walivyomjibu.

Katika Matendo 5:33-39 tunakutana na mwalimu muhimu wa sheria, aliyeitwa Gamalieli. Alikuwa na sifa njema. Watu walimsikiliza wakati alipozungumza. Gamalieli alisimama sasa kuzungumza na baraza. Chora mviringo (au piga mstari) kwa kila sentensi inayoeleza mambo ambayo Gamalieli alisema.

1. Enyi waume wa Israeli, jihadharini jinsi mtakavyowatenda watu hawa.

2. Watu watatudhuru, tukiwadhuru watu hawa.

3. Ikiwa kazi ya mitume ya binadamu, itakuwa bure.

4. Ikiwa Mungu anawaongoza mitume, hamwezi kuvunja kazi yao.

Soma katika Matendo 5:40-42 jinsi baraza lilivyoamuru mitume wapigwe. Pia, waliwaamuru mitume wasifundishe tena habari za Yesu, halafu wakawafungua. Piga mstari chini ya sababu unazojua kuwa mitume walimpenda Yesu sana.

1. Walifurahi kuwa walistahili kuteseka kwa ajili ya Yesu.

2. Walifurahi kwa sababu baraza halikuthubutu kuwafunga gerezani.

3. Waliendelea kufundisha na kuhubiri habari za Yesu

## KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

**"Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu." Matendo 5:29**

## WAKATI WA KUFUNGA

Katika wakati wa kufunga, uwaambie wanafunzi kurudia kifungu cha kukumbuka. Kisha omba ya kwamba Mungu atamsaidia kila mmoja kuwa shujaa na mwaminifu kwa Yesu wakati ambapo ni vigumu kufanya hivyo.

kuwahubiria watu habari za Yesu. Kuhani mkuu alikasirika sana, akawafunga gerezani. Weka alama hii ( X ) kando ya sentensi inayoeleza sababu iliyomfanya malaika wa Mungu kuwafungua mitume wale gerezani.

_____ Mitume wale walitaka kutoka gerezani.

<u>X</u> Mitume wale, baadaye wangeweza kuwahubiria watu habari za Kristo.

Kuhani mkuu aliwatuma maafisa gerezani kuwaleta wale wafungwa. (Matendo 5:21-23) Alishangaa sana wakati aliposikia habari ya maafisa hao. Je! maafisa hao waliwaambia kuhani mkuu na watu wa baraza habari gani?

<u>BARAZA TUMEIKUTA IMEFUNGWA SALAMA, NAO WALINZI WAMESIMAMA MBELE YA MLANGO. LAKINI</u>

<u>TULIPOUFUNGUA HATUKUKUTA MTU NDANI.</u>

Soma Matendo 5:24-26. Kisha, kata maneno yasiyo kweli katika sentensi zifuatazo.

1. Kuhani mkuu, jemadari wahekalu, askari walinzi, na wakuu wa makuhani (walijua) ~~(walikuwa na shaka)~~ kwamba mafundisho ya mitume yangeendelea.

2. Mtu mmoja aliwaambia, "Watu wale mliowaweka ~~(hekaluni)~~ (gerezani) wanafundisha watu (hekaluni) ~~(gerezani)~~!"

3. Jemadari na maafisa waliwaleta mitume ~~(si kwa nguvu)~~ (kwa nguvu). Waliogopa watu (wangewapiga kwa mawe) ~~(wangewasulibisha)~~ kama wangewadhuru mitume wale.

Soma Matendo 5:27-32 umalize kuandika hapo chini swali ambalo






Lakini, muda ule ule walipomjua, akatoweka machoni pao.



Kisha Kleopa na rafikiye wakaelewa sababu ya mioyo yao kuwaka ndani yao wakati Yesu alipozungumza nao. Wakasemezana, "Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa nasi njiani, na kutufunulia maandiko?" Sasa walikuwa na tamaa ya kuwaambia wafuasi wengine habari hii njema. Walirejea upesi Yerusalemu.

Wote wawili waliwakuta mitume wakiwa pamoja ndani ya chumba. Marafiki za Yesu walifunga milango kwa nguvu kwa sababu waliogopa kuwa pengine Wayahudi wangewaua wao pia.

Kleopa na rafiki yake walipoingia mle chumbani, waliwakuta mitume wakisema juu ya ufufuo, kwa sababu Petro pia alikwisha kumwona Yesu.

Walipokuwa wakikaa wote pamoja wakipeana mawazo, Yesu alitokea kwa ghafula na kusimama katikati yao. Akawaambia, "Amani iwe kwenu." Pengine ungefikiri kwamba wafuasi hao wangalikuwa nafuraha kumwona Yesu, lakini sivyo kwa sababu aliingia mle chumbani hali milango ilikuwa imefungwa, kwa hivyo waliogopa mno. Walifikiri ya kwamba alikuwa roho.

Yesu aliwambia, "Mbona mnafadhaika? na kwa nini mnaona shaka mioyoni mwenu? Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikeni-shikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo." (Luka 24:37-39)

Kisha akawaomba chakula, akala mbele yao ili kuthibitisha kwamba alikuwa mtu halisi wala si roho.

Baada ya kula, Yesu akasema nao juu ya Maandiko ya Agano la Kale. Aliwaonyesha jinsi kifo chake na ufufuo wake yalivyotukia kama yalivyoahidiwa na Maandiko.

**KAZI YA KUFANYA**

Siku ya Jumapili asubuhi wanawake walikwenda kaburini. (Luka 24:1-7) Chora mstari kutoka kwa kaburi hadi kwa kila fungu la maneno yaliyo sawa.

Jiwe lilikuwa bado limeziba mlango wa kaburi.




Yesu alikuwa amefufuka kama alivyosema.

Soma Luka 24:8-12. Kisha uchore mstari kutoka kila swali hadi kwa kila jibu lake.

| | |
|---|---|
| Wanawake wale walikumbuka nini? | Yohana na Petro. |
| Waliwaambia watu gani habari yao njema? | Maneno ya Yesu. |
| Ni wafuasi gani ambaye walikimbia kwenda kaburini na kuchungulia ndani? | Walio-staajabia yaliyotukia |
| Kisha walifanya nini? | Wafuasi kumi na moja.. |

Mwokozi aliyefufuka alipo-andamana na watu wale wawili, watu hao hawakumtambua. Chora duara kwa herufi N (ndiyo) kando ya kila fungu la maneno yaliyo sawa, pia uchore duara kwa herufi L (la) kando ya kila fungu la maneno yasiyo sawa.

(N) L Watu wawili walikuwa wakitembea kwenda kijiji cha Emau.

(N) L Watu hao wawili walikuwa na huzuni.

N (L) Yesu alikutana nao na kuwaambia kuwa yeye alikuwa nani.

(N) L Walimwambia Yesu jambo ambalo wanawake wale waliona kaburini.

N (L) Yesu alikaa nao usiku mzima nyumbani mwao.

(N) L Walipomtambua Yesu, alitoweka machoni pao.



Wanaume walitaka kueleza jambo la furaha. Yakate maneno yote yasiyo sawa yaliyoko katika alama hii ( ) Luka 24:32-35.

1. Watu waliambiana, "Je, mioyo yetu (haikuwaka ndani yetu) (~~haikugeuka baridi~~) aliposema nasi?"

2. Wao (walirejea saa ile ile) (~~walikaa kwa muda, kisha wakaenda~~) Yerusalemu.

3. Walirejea upesi kuwaambia (wafuasi) (~~malaika~~) habari yao njema.

4. Wafuasi walikuwa wakisema ya kwamba Yesu alikuwa (amekwisha kufufuka) (~~alikuwa bado yu ngali kaburini~~).

Jifanye kuwa ulikuwako katika chumba kile usiku ule ambapo Yesu aliwatokea wafuasi wake.

Weka alama hii ( X ) kando ya sentensi mbili za kweli ambazo ungekumbuka kuwaambia wengine kuonyesha ya kwamba Yesu alikuwa hai kweli.

_____Mwanzoni wafuasi wake waliogopa.



Mungu aliwazuia viongozi wale kufanya mpango wao wa kuwaua mitume. Mtu mmoja kati yao, ambaye aliitwa Gamalieli, aliweza kuona kwamba viongozi wale wengine walikuwa tayari kuwaua mitume. Basi, aliwatajia jinsi Theuda na Yuda walivyojidai zamani ya kwamba walikuwa wakuu kuliko wengine. Aliwaeleza jinsi kujidai kwao kulivyomalizika bila tendo lo lote la baraza.

Kisha Gamalieli, mwalimu maarufu wa sheria ya Mungu akatoa hoja yake, akisema, "Jiepusheni na watu hawa. Ikiwa juhudi hizi ni za mwanadamu, zitavunjwa; zikiwa za Mungu, hamtaweza kuzivunja. Mkijaribu kuzivunja, mtaonekana kuwa mnapigana na Mungu."

Baraza lilisikiliza kwa makini mashauri haya mazuri, lakini wakakata shauri kwamba hawangewafungua mitume bila kuwaadhibu, basi wakawapiga. Mipigo kama hiyo siku zile, ilikuwa mikali sana hata mara nyingi watu waliopigwa walikufa.

Je! mitume walionyesha hali gani kwa kupigwa kwao? Walikufa moyo? Je! walikata kuacha kazi hiyo? Je! waliwaza kwamba Mungu aliwaonea? La! Walifurahi kwa sababu walihesabiwa kuwa walistahili kudhulumiwa kwa ajili ya Mwokozi wao. Walimpenda Yesu na walijua kwamba alikufa kwa ajili yao.

Je! unafikiri utii wako kwako kwa Kristo unaweza kukufanya kuwa na moyo wa kuteseka kwa ajili yake? Siku hizi ni rahisi kwa watu wengi kuwa Wakristo hapa Afrika, lakini zamani Wakristo wengine wamekufa kwa ajili ya imani yao. Watu wengi wa Asia na Waislamu wanapompokea Kristo kuwa Mwokozi wao hudhulumiwa na kuteswa na jamaa wao wenyewe. Mara kwa mara wazazi wao huwafukuza kutoka nyumbani, kisha wao huwa na shida ya kupata kazi. Wengi hulazimishwa kuoa au kuolewa na watu wasio Wakristo. Hata hivyo, watu hawa hufurahi kuacha mambo haya yote ili kupata uhuru wa kiroho unaopatikana maishani wakati mtu anapompokea Yesu kuwa Bwana wake. Je! unapoteswa na kudhihakiwa kwa kumfuata Kristo, utakuwa kama mitume wale na kufurahi ya kwamba unamtukuza Kristo?

**KAZI YA KUFANYA**

Soma Matendo 5:12-16 uone mambo ambayo mitume walifanya. Chora mstari kutoka kwa neno "mitume" hadi kwa mambo waliyofanya.

MITUME

- Walifanya ishara na maajabu mengi.
- Waliwaimbia watu.
- Waliwaongoza watu wengi kumwamini Bwana.
- Walijaribu kuvunja hekalu.
- Waliwaponya wagonjwa wengi.

Tunasoma katika Matendo 5:17-20 ya kwamba mitume waliendelea

Watu wa baraza waliposikia habari hii ya kushangaza, walistaajabu. Walikuwa wamewafunga mitume gerezani kwa sababu miujiza yao ilikuwa ikiwavuta watu wengi na mafundisho yao yalikuwa yakiwageuza watu wengi kuwa waamini wa Yesu. Na kwa vile sasa walikuwa wameondoka gerezani kwa njia ya ajabu, wangezidi kuwa mashujaa mbele ya macho watu! Badala ya kukomesha kazi yao ilionekana kila kitu walichofanya kilisaidia kazi ya mitume.

Watu wa baraza walipokuwa wakifikiria jambo la kufanya, mtumishi mmoja aliwaletea habari ya kuwaudhi sana. Soma habari hiyo katika Matendo 5:25.

Muda si muda, jemadari wa hekalu na maafisa waliwaleta mitume wale mbele ya baraza. Lakini watawala hawakuthubutu kuwaua kwa sababu walijua watu waliwapenda mitume zaidi mno hata wangeweza kuwapiga kwa mawe kama wangejaribu kuwadhuru watu hawa wa Yesu. Baada ya watawala kuona uwezo wa Mungu katika kuwafungua mitume wale gerezani na kuwafanya kuwa huru, inaonekana kama kwamba wangaliogopa jambo ambalo Mungu angewafanyia kama wangewadhuru watumishi wake. Lakini, wao waliamini ati mitume wale walikuwa waovu.

Kuhani mkuu alikasirika sana, akawaambia mitume wale, "Tuliwaamuru ninyi kwa nguvu msifundisha kwa jina la Yesu. Lakini, badala yakututii sisi mmeijaza Yerusalemu mafundisho yenu. Mnawaambia watu ya kwamba tuna hatia ya kumwua Yesu."

Ndiyo, huu ndio uliokuwa ukweli. Mitume wale walifanya kama alivyosema. Petro alijibu shtaka la yule kuhani mkuu kwa kumwambia ya kwamba alikataa kumtii kwa sababu ya amri alizopata kutoka kwa mkuu (Mungu). Hiki ndicho kifungu chetu cha kukumbuka leo.

Mungu ametwambia kuwatii viongozi wetu. Tunaweza kusoma amri hii katika Warumi 13:1. Basi, kwa nini mitume wale walikataa kuwatii viongozi wao? Mitume wale hawakuweza kutii amri ya Mungu na amri ya viongozi wao. Mungu alikuwa amewaambia kuhubiri habari za Yesu Kristo kwa watu wote; lakini viongozi wale walikuwa wamewakataza kusema wala kufundisha habari za Kristo. Mitume hawangeweza kutii amri hizi zote mbili, ya Mungu na ya viongozi wale. Mitume walichagua kumtii Mungu.

Petro hakunyamaza baada ya kujibu. Alipata nafasi ya kuwahubiria watu wa baraza lile. Aliendelea kwa haraka kuwaambia ya kwamba Kristo ambaye walimwua kwa kumsulibisha msalabani, alikuwa amefufuliwa katika wafu na kutukuzwa na Mungu.

Viongozi wale walipokuwa wakimsikiliza Petro akiwahubiri, walijiona kuwa wenye hatia na dhambi lakini hawakutaka kukubali hatia yao, kwa hivyo walipanga kuwaua mitume wale.



____Walifikiri kuwa Yesu alikuwȧ roho.

__X__Yesu aliwaonyesha wafuasi wake mikono na miguu.

__X__Yesu alikula mbele yao kuonyesha ukweli kwamba yeye hakuwa roho.

**KIFUNGU CHA KUKUMBUKA**

**"Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko; na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko." 1 Wakorintho 15:3b, 4**

**WAKATI WA KUFUNGA**

Wakati ambapo wanafunzi watakuwa wamemaliza kazi zao katika somo lao, waambie wasikilize tena.

(Sema:) Yesu alipofufuka katika wafu, wafuasi wake walikuwa na furaha sana. Ufufuo wake ulikuwa wa maana sana kwao. Je! ufufuo huo wake ni wa maana kwako leo? Ikiwa una maana kwako, basi eleza ni kwa nini? (Waache wanafunzi wajibu.)

Kama Yesu hangefufuka katika wafu, je! kifo chake msalabani kingeweza kuondoa dhambi zako? La, kifo cha Yesu kingalikuwa kama cha mtu ye yote tu wa kawaida kama hangalifufuka tena. Alitoka kaburini, akiwa hai kwa hivyo tunajua ya kuwa yeye ni Mwana wa Mungu. Kifo chake kinamkomboa kila mtu anayeamini kwake.

Je! unamwamini Yesu? Unaamini kwamba yuko hai sasa? Unataka kumjua Bwana huyu aliye hai ambaye anaweza kukukomboa? Siku ya leo ndiyo siku inayokupasa wewe kumwamini.

Funga kwa maombi.

# MTU ALIYEAHIDIWA

**MASOMO YA BIBLIA: Yohana 14:16-28; 15:26-27; 16:7-15; Matendo 2:1-11**

## KUJIANDAA KUFUNDISHA

Yesu aliahidi kwamba Roho Mtakatifu angekuja na kuwa na kazi fulani ya kufanya. Waeleze wanafunzi wako wakati wa somo hili ya kwamba neno lake Yesu lilitendeka jinsi alivyosema. Roho Mtakatifu alikuja. Pia wasaidie wanafunzi kutaka Roho Mtakatifu aje katika maisha yao na kufanya kazi yake ndani yao. Mara nyingi twajaribu kuwafundisha wanafunzi jinsi wanavyopaswa kuonyesha tabia, lakini twasahau kuwaonyesha jinsi Bwana atakavyowasaidia kutenda mambo kwa njia inayowapasa

Kusudi la somo hili ni kueleza jinsi Mungu alivyotoa msaada wake kutusaidia, akitupa Roho Mtakatifu kuishi ndani yetu na kututawala.

## MAMBO YA KUKAZA

1. Bwana wetu Yesu anaishi ndani ya mioyo ya waamini kwa njia ya Roho Mtakatifu.

2. Wakati ule wa Pentekoste, Roho Mtakatifu aiwapa wafuasi wa Yesu ishara ya kuja kwake na uwezo wa kusema kwa lugha nyingine.

3. Wakristo ambao wanamruhusu Roho Mtakatifu kuwaongoza, wanageuka kama Kristo.

## KULIFUNDISHA SOMO

Anza darasa kwa maombi katika wimbo. Yaani, wanafunzi wote wainamishe vichwa vyao, wafumbe macho na kuimba.

### NDANI YA MOYO WANGU

Moyoni mwangu,
Moyoni mwangu
Njoo Yesu,
Moyoni mwangu
Uje sasa, uje kukaa.
Njoo Yesu,
Moyoni mwangu.

Kisha uombe ombi hili fupi kama bado wanafunga macho yao: "Ee Bwana, utusaidie leo tuweze kuelewa jinsi unavyoweza kuja kukaa ndani ya mioyo yetu."

Uliza maswali haya: Mkristo ni mtu gani? Je! unaweza kujua ikiwa mtu ni Mkristo? Ikiwa unaweza, je! ni kwa jinsi gani? Je! ni jambo gani maishani mwa mtu ambalo linaweza kuwa dalili kwamba ameamini kwake Yesu.?

Waache wanafunzi wazungumze bila kuwazuia. Usikubali au kuyakataa mawazo yao. Somo lenyewe linawasaidia kukata shauri kama wana mawazo mazuri au la.

(Sema:) Hebu tujifanye kama kwamba tu kikundi cha wafuasi ambao Yesu aliacha alipopaa mbinguni. Tuliambiwa kungojea Yerusalemu mpaka wakati ambapo



kumtii Mungu kuliko kuwatii wanadamu.

Mungu alijibu maombi ya mitume wale waliomwomba ushujaa. Waliendelea kwenda kanisani kuhubiri. Ujumbe wao uliwavuta wengi, na watu wengi walimpokea Yesu kuwa Mwokozi wao. Habari kuhusu uwezo wa Petro wa kuponya zilienea kwa kila nyumba Yerusalemu na katika miji ya karibu. Tazama Matendo 5:15-16, uone mambo ambayo watu walifanya ili kuwafanya marafiki wao kuponywa.

Viongozi wa kidini walikuwa wamekwisha kuwaonya Petro na Yohana kuacha kuhubiri katika jina la Yesu. Waliposikia kwamba mitume wale walikosa kuwatii, walikasirika sana. Watawala waliwafunga mitume wale gerezani.

Walakini, hawakukaa gerezani kwa muda mrefu. Usiku ule malaika wa Bwana alifungua milango ya gereza, akawatoa nje. Kama desturi



wafungwa wengi wanapotoroka gerezani hujificha wasikamatwe tena. Lakini malaika aliwaambia mitume hawa kurudi hekaluni ambako walikuwako mwanzoni na kuhubiri ujumbe ule ambao uliwafanya kukamatwa.

Mitume walitii. Ilipokuwa alfajiri walirudia kazi yao ya kuwafundisha watu habari za Yesu Kristo.

Je! unafikiri walijua kwamba wangejiletea shida zaidi kwa kuendelea kuhubiri? Ndiyo walijua. Ni nini basi iliyowafanya kuwa mashujaa na kuanza kuhubiri tena? Ingawa walijua kwamba watu wangewakamata, walijua kwamba Mungu wao alikuwa mkubwa kuliko mamlaka yo yote ambayo mwanadamu angetumia kuwatawala.

Kwa wakati huu, makuhani wakuu walifanya mkutano wa baraza kukata shauri kama wangefanya nini kuhusu mitume wale. Waliwatuma maafisa gerezani kuwaleta mitume mbele zao.

Maafisa wale walipofika gerezani, walishangaa kuona gereza likiwa tupu, wafungwa walikuwa wameondoka. Hawakuwa wametoroka kwa sababu ya uvivu wa askari walinzi kwa kuwa gereza lilikuwa limefungwa salama.

Maafisa wale walirudi kwa baraza, wakawapasha habari hii: Walisema, "Gereza tumeikuta imefungwa salama, nao walinzi wamesimama mbele ya mlango; lakini tulipoufungua hatukukuta mtu ndani." (Matendo 5:23)

# MASHAHIDI GERAZANI

**MASOMO YA BIBLIA: Matendo 5:12-42**

### KUJIANDAA KUFUNDISHA

Mambo mengi husemwa siku hizi katika Afrika kuhusu "uhuru." Yesu anasema ya kwamba uhuru wa kweli hutokana na kumjua yeye na kutii neno lake. Ni kwa sababu hii ndiyo watu wengi katika nchi za Kikomunisti siku hizi wangali wanaweza kuwa na "uhuru" mioyoni mwao ingawa wanaweza kuwa gerezani kwa "hatia" ya kuwa Wakristo. Katika somo hili tunaona ya kwamba mitume ya kwanza pia walikuwa na uhuru wao wa kiroho, hata wakati walipokuwa gerezani.

Kusudi la somo hili ni kuwaonyesha wanafunzi ya kwamba mitume walimtii Bwana kuliko kuwatii wanadamu. Wasaidie kukata shauri kwamba wao pia inawapasa kumtii Mungu hata kama kufanya hivyo kutahatarisha maisha yao.

### MAMBO YA KUKAZA

1. Kanisa liliongezeka wakati mitume walipoomba kupewa ushujaa.

2. Bwana aliwaokoa mitume gerezani na kuwarudisha hekaluni.

3. Mitume walinena ya kwamba walikuwa wamejitoa kumtii Mungu kuliko kutii utawala wa mwanadamu.

4. Mungu aliwapa ushujaa wa kumtii.

### KULIFUNDISHA SOMO

**Wanafunzi wako wote wakiwa na Biblia, uwaambie wasome pamoja Zaburi 25:4-5. Ikiwa hawana Biblia, uwasomee yako. Uliza swali hili: Je! mnapata shida kufanya jambo ambalo mnajua Mungu anataka mfanye?**

**(Andika swali hili ubaoni au kwenye kipande kikubwa cha karatasi:) Nawezaje kumtii Mungu hata wakati ambapo ni vigumu kufanya hivyo?**

**Ulijifunza katika somo lililopita ya kwamba Petro na Yohana walikuwa wameonywa na baraza wasiendelee kufundisha habari za Yesu. Baada ya mitume wale kuachiliwa huru, walirudi kwa marafiki wao, wakaomba pamoja. Je! mitume wale walimwomba Mungu kuwalinda au kuwapa kazi rahisi? Tazama Matendo 4:29-30, uone kwamba waliomba wakitaka nini. Ndiyo, walimwomba Mungu kuwapa ushujaa wa kuhubiri, na uwezo wa kufanya miujiza katika jina la Yesu.**

**Walimpenda Yesu sana hata hawangeacha kuwaambia watu habari zake. Kwa hivyo, walimwomba Mungu kuwapa ushujaa wa kumshuhudia Yesu bila kujali cho chote ambacho kingetukia.**

**Uaminifu kwa Kristo wakati wa hatari si rahisi, lakini Roho Mtakatifu huwaimarisha wale walio na nia ya**



Roho Mtakatifu angekuja. Na kwa kuwaogopa viongozi wa Wayahudi, tulikutanika ndani ya chumba tukiwa tumefunga milango. Tulijaribu kuzungumza juu ya jambo ambalo lilitupasa kufanya ili kuonyesha ulimwengu kuwa tu wafuasi wa Kristo. Hatungekuwa na Agano Jipya la kutuongoza, au mchungaji, au waalimu, wala makanisa kwa maana Yesu alikufa kama mhalifu. Tu kikundi kidogo tu cha watu. Tunajua ya kuwa Yesu alikuwa amefufuka katika wafu, lakini karibu kila mmoja anafikiri kuwa tunadanganya juu ya jambo hilo. Labda tunaweza kuadhibiwa kwa kusema juu ya imani yetu katika Yesu.

Shida hizi zote, kweli zilikuwa shida kubwa kwa wafuasi wa Yesu. Hawakujua jambo la kufanya. Wangalifanya imani yao kuwa siri na kutomwambia mtu ye yote, lakini kwa njia hiyo wangalikuwa wanavunja amri ya Yesu kwa wao kumhubiri katika ulimwengu. Alikuwa amesema, "Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi." (Mathayo 28:19-20)

Jambo hilo lilionekana kuwa gumu mno kwa wafuasi.

Hebu turejee wakati ambao Yesu alisema na wafuasi wake kabla hajatoa maisha yake msalabani. Kwa miaka mitatu alikuwa kiongozi wakikundi hicho kidogo. Lakini sasa alijua kwamba, baada ya muda wa siku mbili angetundikwa msalabani, na wafuasi hao wake wangeachwa peke yao. Walihitaji mtu mwingine wa kuwasidia. Alijua ya kwamba angefufuka, lakini hangeweza kukaa nao kwa muda mrefu. Kazi yake sasa ingekuwa imemalizika, na angeweza kurudi kwa Baba yake mbinguni.

Yesu alizungumza juu ya kuondoka kwake wakati kikundi cha wafuasi wake walipokaa naye mezani wakila pamoja chakula cha mwisho cha Sikukuu ya Pasaka. Bila shaka wafuasi walikuwa na wasiwasi kwa sababu walifikiri hawangeweza kuendelea na kazi yao bila kuwa pamoja na Yesu. Walikuwa wamemtegemea yeye, naye alikuwa amewapa maongozi, ushujaa, na tumaini.

Yesu alijua kwamba hawangeweza kufanya kazi yake kwa nguvu zao wenyewe. Tena alikjua kwamba ulikuwa mpango wa Mungu kwao kuwa na msaada. Kwa hivyo, aliwaahidi, "Sitawaacha ninyi yatima; naja kwenu." (Yohana 14:18) Baada ya kurudi kwake mbinguni, Yesu alipanga kuja kwa wafuasi wake kwa njia ya Roho Mtakatifu.

Roho Mtakatifu ni nani? (Waache wanafunzi wajaribu kujibu.)

Kuna watu watatu katika Utatu Mtakatifu: Baba, ambaye tunamwita Mungu; Mwana, Yesu Kristo; na Roho Mtakatifu. Kila mmoja wao katika utatu huo ni sawa ma mwenziwe. Wote ni mmoja, walakini kila mmoja wao ana tabia zake mwenyewe.

Yesu aliwaambia wafuasi wake juu ya Roho Mtakatifu ambaye angewatumia. Angalia katika Yohana 14:7. Tazama mahali ambapo Roho Mtakatifu angekaa; angekaa ndani ya waamini, sio ndani ya mitume peke yao, lakini ndani ya waamini wote.

Pengine Mitume waliogopa ya kwamba wangesahau vitu vingi kati ya yale muhimu ambayo Yesu aliwafundisha. Angalia katika Yohana 14:26, uone jinsi Yesu alivyojibu shida hii. (Roho Mtakatifu angewasaidia kukumbuka vitu vyote walivyofundishwa na Yesu.)

Pengine walifikiria jinsi wangeweza kuwavuta watu kuamini ujumbe wao. Yesu aliahidi kwamba Roho Mtakatifu angefanya kazi ndani ya mioyo ya waume na wanawake, wavulana na wasichana, kuwaonyesha jinsi ilivyo dhambi kukataa kumpokea Yesu kama Mwokozi wao. Roho Mtakatifu pia angewasaidia watu kuona kwamba njia ya pekee ambayo wanaweza kuwa wenye haki machoni pa Mungu ni kumwamini Yesu. Kisha, waamini wangeweza kuwa na ushindi juu ya Shetani kwa uwezo wa Roho Mtakatifu maishani mwao.

Siku kumi baada ya Yesu kurudi kwa Baba yake aliye mbinguni, wafuasi wake wote walikuwako mahali pamoja wakiomba. Na kwa sababu ilikuwa sikukuu ambayo ilikuja siku hamsini baada ya Pasaka, iliitwa Pentekoste, maana yake "Hamsini". Kwa ghafula, mahali pale pote ambapo wafuasi walikuwako wakiomba palijaa uvumi ambao ni kama uvumi wa upepo wa nguvu. Na wakati ule ule, kila mfuasi aliona ndimi zilizogawanyikana kama ndimi za moto juu ya vichwa vya wafuasi wengine. Hizi zilikuwa ishara za kuonyesha kwamba roho Mtakatifu alikuwa amekuja kuishi ndani ya waamini kama Yesu alivyoahidi.

Wafuasi walianza kusema kwa lugha nyingine ambazo hawakuzijua. Kwa upesi makutano ya watu walikusanyika. Walikuwa wamesikia uvumi kama wa upepo, na walikuja kuona kama ulikuwa nini. Katika makutano wale walikuwako Wayahudi kutoka kila taifa ambao walisema lugha mbalimbali.



Walistaajabu waliposikia wafuasi wakisema kwa lugha zao.



Yesu alikuwa amewaamuru wafuasi wake kwenda kwa kila taifa na ingawa hapa walikuwa bado wako Yerusalemu. Lakini walikuwa wamekwisha kuanza kueneza habari



Siku chache baada ya Pentekoste, hesabu ya waamini iliongezeka ikawa kama (5,000) (~~1,000~~).

Katika Matendo 4:5-7 tunasoma habari za watu muhimu ambao walikuwa katika baraza la Wayahudi. Katika mistari hiyo hapo chini, andika swali ambalo watu hao waliwauliza Petro na Yohana.

Kwa nguvu gani na kwa jina la nani ninyi mmefanya haya?

Soma Matendo 4:13-17, kisha piga mstari chini ya jibu sawa la kila swali.

Je! kwa nini watu wa baraza lile walishangaa?

a. Waliwaona Petro na Yohana kuwa kama Yesu.

b. Walijua ya kwamba, ingawa Petro na Yohana hawakuwa na elimu, walisema kwa uwezo kama Yesu alivyosema.

Watu wa baraza lile waliwaamuru Petro na Yohana kutoka nje wakati walipokuwa wakifanya shauri juu ya jambo la kufanya. Je! shida yao ilikuwa nini?

a. Labda kiwete yule aliyeponywa angesema kwamba hakuponywa kabisa.

b. Kiwete yule aliyeponywa alikuwa akisimama pale, kwa hivyo hawangeweza kukana mwujiza ule.

Soma juu ya mambo yaliyofanyika tena katika Matendo 4:18-20. Sasa chora mstari kutoka mambo yaliyosemwa hadi kwa mtu aliyeyasema.

"Msiseme kabisa na kufundisha kwa jina la Yesu."

"Kwamba ni haki mbele ya Mungu kuwasikiliza ninyi kuliko Mungu, hukumuni ninyi wenyewe. Maana sisi hatuwezi kuacha kuyanena mambo tuliyoyaona na kuyasikia."




Soma juu ya maamuzi ya Baraza katika Matendo 4:21-22. Piga mstari chini ya jibu lililo kweli.

Baraza halikuwaadhibu Petro na Yohana kwa sababu:

a. Watu wote walimsifu Mungu kwa kumponya kiwete.

b. Watu waliwalinda Petro na Yohana.

### KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

**"Iweni hodari na moyo wa ushujaa, msiogope wala msiwahofu; kwa maana Bwana, Mungu wako, yeye ndiye anayekwenda pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha." Kumbukumbu la Torati 31:6**

### WAKATI WA KUFUNGA

Funga darasa kwa maombi. Omba ili kwamba nyote mtaweza kuwa na ushujaa wa kuwa waaminifu kwa Kristo bila kujali hatari yo yote au dhihaka za watu.

sheria yo yote waliyopewa na baraza kuu.

Petro aliwashangaza watawala hao kwa kusema, "Kwamba ni haki mbele za Mungu kuwasikiliza ninyi kuliko Mungu, hukumuni ninyi wenyewe; maana sisi hatuwezi kuacha kuyanena mambo tuliyoyaona na kuyasikia." (Matendo 4:19b-20)

Tafuta katika Matendo 1:8 kwa nini mitume wale hawakutii baraza. Kristo alikuwa amewaamuru kuwa mashahidi wake mahali po pote waendapo.

Je! Petro na Yohana walikwisha kusikia na kuona Yesu akifanya nini? Kila siku walimsikia akihubiri na kufundisha; walimwona akiwasaidia maskini na wagonjwa; walimwona akifa msalabani; walimwona akiwa hai baada ya kufa; na walimwona akipaa juu mbinguni.

Ni siku chache zilizopita ambapo Yesu mwenyewe alikuwa ameletwa mbele ya makuhani hawa wakuu na watawala. Je! unakumbuka mahali Petro alikuwapo na jambo lililokuwa akifanya wakati Yesu alipokuwa hukumuni? Alisimama nje pamoja na watumishi, na alimkana Yesu mara tatu ya kwamba hakumjua.

Lakini sasa, Petro mwenyewe alikuwa akisimama mahali pale pale ambapo Bwana wake alisimama siku chache zilizopita. Bila shaka Petro alikumbuka usiku ule ambapo alimkana Yesu, na bila shaka alistaajabia ushujaa aliokuwa nao sasa kwa kukataa kutii baraza lile.

**Nani aliyebadilisha hali ya Petro ya uwoga na kumfanya kuwa mtu mkubwa na shujaa? Ni Roho Mtakatifu!**

**Baraza liliwaogopa watu kwa hivyo hawakuwaadhibu Petro na Yohana. Walijaribu kuwatisha kwa kuwaambia kwamba wangeteseka kama wangehubiri tena habari za Yesu.**

**Wape wanafunzi wakati wa kuuliza maswali juu ya somo hili. Wakitaka kuzungumza, uwaruhusu kufanya hivyo. Kisha sema, "Unawezaje kuwa mwaminifu kwa Kristo ukikaa na watu ambao hawamjui Yesu?" Kifungu chetu cha kukumbuka cha leo kinatwambia jinsi unavyoweza kufanya hivyo.**

**KAZI YA KUFANYA**

**Soma Matendo 4:1-4, kisha kata maneno yasiyo kweli katika sentensi zufuatazo:**

**Petro na Yohana walikuwa wakisema na watu. Mara (makuhani) na ~~(manabii)~~ (akida wa hekalu) na (Masadukayo) walifika.**

**Viongozi hawa ~~(walifurahi)~~ (walikasirika) kwamba Petro na Yohana walikuwa wakihibiri juu ya Yesu ufufuo wa wafu.**

**Kwa sababu ilikuwa jioni waliwaweka Petro na Yohana gerezani mpaka ~~(wiki iliyofuata)~~ (asubuhi).**

**Wengi kati hao (walimwamini Yesu) ~~(waliwaokoa)~~.**



njema ya Yesu Kristo. Baada ya sikukuu, watu wale ambao waliwasikia wafuasi walirudi katika nchi zao wakawaambia wengine habari ya kuona kwao na kuwasikia wafuasi hao wa Yesu wakisema "matendo makuu ya Mungu" kwa lugha nyingi (Matendo 2:11).

Je! watu watatu hawa wa Utatu Mtakatifu hufanyaje kazi pamoja kutufanya sisi kuwa watoto wa Mungu?

1. Mungu Baba anatupenda mno akamtuma Mwanawe ulimwenguni kufa kwa ajili yetu sisi.

2. Mungu Mwana anatupenda sana hata akajitoa yeye mwenyewe binafsi kama sadaka ya pekee ambayo ingeweza kuondoa dhambi zetu.

3. Mungu Roho Mtakatifu anatupenda sana hata anafanya kazi mioyoni mwetu wakati ambapo hatujampokea Yesu kama Mwokozi wetu na pia baada ya kumpokea, ili kutufanya kuchukia dhambi.

Kabla hatujampokea Kristo, Roho Mtakatifu hufanya kazi yake juu yetu ili tuweze kumpokea. Na baada ya sisi kuzaliwa mara ya pili, yeye sasa hufanya kazi ndani yetu. Kabla ya sisi kumwamini Yesu, Roho Mtakatifu hutufanya kutambua kuwa tu wenye dhambi mbele za Mungu. Kisha mara tutunapozaliwa mara ya pili, Roho Mtakatifu hukaa ndani ya mioyo yetu kutusaidia kuishi kama Wakristo wa kweli.

**KAZI YA KUFANYA**

Je! Yesu alisema nini juu ya Roho Mtakatifu? Weka alama hii ( X ) kando ya kila fungu la maneno lililo kweli. Yatafute majibu katika vifungu vyako vya Biblia iwapo huyajui.

Yohana 14:16

_X_ Atakaa na wafuasi milele.

____ Ataakaa nao kwa muda kisha hawatamwona tena.

Yohana 14:26

_X_ Atawafundisha mambo yote.

_X_ Atawakumbusha yote yaliyosemwa na Yesu.

Yohana 15:26

____ Atawafanyia wafuasi kazi yao.

_X_ Atamshuhudia Yesu.



Wafuasi wote walikuwa wakikaa pamoja katika chumba kikubwa. Kwa ghafla, Roho Mtakatifu akawajia.

Walisikia nini? Walisikia kishindo kama uvumi wa upepo.

Ni kitu gani kilichokuwa juu ya kichwa cha kila mmoja wao? Ndimi za moto.

Roho Mtakatifu aliwapa wafuasi uwezo wa ajabu. Weka alama hii (X) mbele ya kila fungu la maneno yaliyo sawa.

_X_ Walianza kusema kwa lugha nyingine.

_X_ Makutano ya Wayahudi waliokuwa wakizuru Yerusalemu kutoka kila taifa walikuja kuwasikiliza wafuasi.

____ Wafuasi walijigamba mbele ya kikundi kile kwamba waliweza kusema kwa lugha za kigeni.

____ Viongozi wa ndini walifurahi kwamba Roho Mtakatifu alikuwa amekuja.

Wayahudi kutoka mataifa mengi ya kigeni walistaajabia jinsi wafuasi waliweza kusema kwa lugha zao.

Wafuasi walisema juu ya jambo gani? Walikuwa wakisema juu ya matendo makuu ya Mungu.

**KIFUNGU CHA KUKUMBUKA**

**"Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?"**
**1 Wakorintho 3:16**

**WAKATI WA KUFUNGA**

**Je! Mkristo ni nani? Ikiwa una ubao wa kuandikia, andika jambo hili kwenye ubaohuo au uliandike mapema katika kipande kikubwa cha karatasi.**

**Mkristo ni mtu:**

**--ambaye anatambua ya kuwa yeye ni mwenye dhambi asiye na tumaini, na ambaye ameamini kwa Yesu kama yule anayeweza kumwokoa.**

**--ambaye ana Roho Mtakatifu anayeishi ndani yake kumfanya kuwa kama Kristo.**

**--ambaye anamtegemea Roho Mtakatifu kila saa kumsaidia kupenda na kutii Neno la Mungu.**

**Bila shaka, Yesu huwa na huzuni nyingi sana kila wakati tunapoikubali dhambi kuingia maishani mwetu na hali ametupa Roho Mtakatifu kutusaidia.**

**Funga kwa maombi.**



Petro na Yohana waliletwa mle chumbani. Kiwete yule waliyemponya pia alikuwapo pale. Kisha wanafunzi hawa waliulizwa, "Kwa nguvu gani mmemponya mtu huyu?" Maadui wa Yesu walitamani kupata nafasi ya kuthibitisha kwamba hapakuwapo mwujiza na kuponya, lakini hawakuweza kufanya hivyo kwa sababu kiwete yule aliyeponywa alikuwa akisimama mbele yao. Baraza lilitaka kuwaadhibu mitume wale na kukomesha mahubiri yao, lakini hawakujua jinsi ya kufanya hivyo

Je! kwa kawaida ni kwa nini watu hukamatwa na kupelekwa kuhukumiwa? Ndiyo, kwa sababu mtu fulani huwafikiria kuwa na hatia ya kosa fulani. Lakini Petro na Yohana walipelekwa mahakamani kwa kutenda mema. Kiwete yule mwombaji aliweza kutembea kwa msaada wao. Kwa ushujaa ambao Roho Mtakatifu alimpa, Petro aliwaambia baraza, "Mkitaka kujua jinsi tulivyomponya kiwete huyu, tutamwambia ninyi na watu wote wa Israeli. Ni kwa uwezo wa Yesu Kristo wa Nazareti, yule mlimsulibisha, na ambaye Mungu alimfufua katika wafu na ndiye alimponya mtu huyu anasimama hapa mbeleni yenu akiwa katika afya njema."

Baada ya Petro kuambia baraza ya kwamba walitenda dhambi mbaya mno kwa kumsulibisha Mwana wa Mungu, aliwaambia habari za upendo wa Mungu ambao habari za upendo wa Mungu ambao ni mkubwa kuliko dhambi zote za wanadamu. Yesu, ambaye walimwua alikuwa na tamaa ya kuwaokoa katika dhambi zao.

Ikiwa hakutaka kumpokea Kristo kuwa Mwokozi wao, je! Mungu alikuwa na mpango mwingine au mtu mwingine ambaye kwake angeweza kuwaokoa? La. Yesu Kristo pekee ndiye Mwokozi. Mungu hatoi njia nyingine. Shauri muhimu zaidi ambalo mtu ye yote anaweza kukataa ni kumpokea Bwana Yesu au kumkataa. Petro alikuwa akisema kwamba kama watu hawa walimkataa Yesu, hawangeweza kuokolewa katika dhambi zao.

Petro na Yohana walikuwa wafungwa wa ajabu. Walikuwa na elimu chache, lakini walijitetea kwa ushujaa na tumaini. Baraza lilitambua ya kwamba walikuwa pamoja na Yesu, kwa sababu walisema kwa uwezo na ushujaa kama ule wa Yesu.

Baada ya kuwaamuru Petro na Yohana kutoka chumbani, baraza lilizungumza juu ya jambo lile. Kama ungalikuwa pale, ungaliwasikia wakisema, "Tuwafanyieni watu hawa? Kiwete huyu ameponywa. Kila mmoja anayekaa Yerusalemu amekwisha kusikia habari hii. Hatutaki watu wengi kuwa wafuasi wa Yesu, kwa hivyo, tuwaonye Petro na Yohana wasimwambie tena mtu ye yote habari za Yesu."

Watawala hao waliamuru Petro na Yohana waletwe chumbani mbele ya baraza. Waliwaamuru wasiseme kabisa wala kufundisha kwa jina la Yesu. Kwa kawaida, watu walitii

(Andika swali hili ubaoni au kwenye kipande cha karatasi.)

Siku moja, wakati wa saa tisa ya alasiri, jambo fulani lilifanyika katika Mlango Mzuri nje ya hekalu. Petro alikuwa amepewa uwezo na Yesu kumponya kiwete aliyeketi pale mlangoni kuomba.

Kama kawaida, watu wengi waliojaa udadisi waliwakusanyikia Petro na Yohana na kiwete yule. Ilipofika jioni, Petro na Yohana walikuwa bado wakisema na watu wale habari za Yesu.

Kwa ghafula, askari walitokea na kuwakamata wanafunzi wale. Maadui wa Yesu walikuwa wamekasirika kwa sababu mitume hawa wawili walikuwa wakihubiri habari ya Yesu. Walifikiri ati walikuwa wamekwisha kumkomesha Yesu kabisa wakati walipomwua. Sasa marafiki wa Yesu walikuwa wakisema kwamba alikuwa hai, na watu wengi walikuwa wakiwaamini.

Akida wa hekalu alikasirika sana juu ya mambo yaliyotokana na kuponywa kwa kiwete yule mwombaji. Masadukayo ambao walikuwa viongozi wa Wayahudi, na ambao walifikiri kwamba hakukuwapo ufufuo wa wafu, pia walifurahi kuwafunga wanafunzi wale gerezani. Walikasirika sana kuwasikia mitume Petro na Yohana wakiwaambia watu kwamba Yesu alikuwa hai.

Makuhani wengine wa Kiyahudi pia walisaidia kuwakamata mitume wale. Ni wao ndio waliowaongoza umati wa watu kumtaka Pilato aamuru Yesu auawe. Walifikiri ati wakati ule walipomwua Yesu kwa kumsulibisha msalabani ndio ungekuwa mwisho wake.

Basi, Petro na Yohana waliwekwa gerezani usiku ule. Baraza lilipanga kuwahukumu kesho yake asubuhi.

Siku ile ambapo Petro na Yohana waliwekwa gerezani, kuhani mkuu na jamaa yake yote na watawala na wazee na waandishi, walifanya baraza la kuwahukumu mitume wale. Labda hili lilikuwa baraza la wazee sabini na mmoja walioshughulika na mambo ya dini. Ni baraza hili ndio waliomhukumu Yesu kufa.







# MAHUBIRI YENYE NGUVU

**MASOMO YA BIBLIA: Matendo 2:12-47**

## KUJIANDAA KUFUNDISHA

Kila mmoja anapenda kusikia hadithi juu ya mashujaa! Tunafurahi kujua habari za watu wanaofanya mambo ya kusisimua. Somo hili ni juu ya Mkristo mmoja shujaa. Petro anatumia uwezo wa roho Mtakatifu kuwa mmojawapo wa wahubiri wakuu. Hadithi juu yake ni ya kusisimua sana, lakini usipoiona kama inakusisimua, watoto hawataifurahia.

Kabla hujaanza, omba ili Bwana atakutumia wewe kusimulia hadithi juu ya mwanafunzi huyu na mambo ya ajabu aliyoyafanya kwa utukufu wa Mungu. Je! hadithi hii ina maana yo yote kwako? Omba ili uweze kuwa na tamaa ya kushiriki watoto wako hadithi hii jinsi Roho Mtakatifu alivyofanya kazi maishani mwa Petro.

Wakristo wengine hata hawajui habari za Roho Mtakatifu. Je! wewe unajua habari zake? Wakati unapompokea Kristo kuwa Mwokozi wako, Roho wake Mtakatifu huingia maishani mwako na kufanya kazi ili kukufanya kuwa kama Kristo. Wakristo wengine, kwa kweli hawajui kwamba Roho Mtakatifu hukaa ndani ya roho zao. Lakini Mungu anataka tujue habari kuhusu kipawa hiki cha ajabu kwa waamini.

Wewe kama mwalimu, unaweza kuona Roho akifanya kazi ndani ya wanafunzi wako. Ukitafuta kuona uso wa Mungu na kujitoa kwake kwa utumishi wake, kwa hakika atakutumia. Amini ya kwamba Bwana atafanya kazi ndani ya mioyo ya wanafunzi wako ili watataka kuwa mashahidi wake bora.

Kusudi la somo hili ni kuwafundisha wanafunzi ya kwamba Roho Mtakatifu atawapa uwezo wa kufanya kazi yake.

## MAMBO YA KUKAZA

1. Roho Mtakatifu alimpa Petro ujumbe na uwezo wa kuhubiri ujumbe huo.

2. Roho Mtakatifu aliwathibitishia wasikilizaji dhambi walizomtenda Yesu, ambazo zilifanya ushuhuda wa Petro kuwa wenye nguvu.

3. Roho Mtakatifu atatutumia sisi kama mashahidi wenye nguvu kama tukimtegemea yeye.

## KULIFUNDISHA SOMO

Darasa lililopita tulisikia ya kwamba umati wa watu uliwazunguka wanafunzi baada ya Roho Mtakatifu kuwajia. Wengine walipaza sauti zao wakisema, "Watu hawa wamelewa."



Mara, Petro alisimama. Umati ule wa watu wakanyamaza kwa sababu walitaka Petro kuwaeleza mambo yale ya ajabu yaliyokuwa yakifanyika. Wanafunzi wengine kumi na mmoja walisimama karibu na Petro wakati alipokuwa akisema. Kabla ya Petro kuwaambia watu mambo yaliyofanyika, aliwaonyesha jinsi walivyokuwa wapumbavu kwa kuwashtaki ati walikuwa wamelewa. Ilikuwa saa tatu tu ya mchana. Katika siku za karamu ilikuwa kinyume cha sheria kwa Wayahudi kula chakula kabla ya wakati ule, wala kunywa.

Watu walipokuwa wakisikiliza Petro alieleza kwamba mambo yale yaliyofanyika siku ile ni yale nabii Yoeli alisema kwamba yangetukia. Kwa hivyo, hawangestaajabia mambo hayo waliyoyaona kama wangekumbuka na kuyaamini maandiko ya Agano la Kale. Petro aliwakumbusha juu ya mambo ambayo Yoeli alikwisha kuyasema.

Mungu alikuwa amewaambia watu wake kwa nabii Yoeli kwamba katika siku za mwisho, yaani, katika siku za Yesu Kristo, angetoa Roho wake Mtakatifu.

Baada ya maelezo yake, Petro alianza mahubiri yenye nguvu. Roho Mtakatifu alitumia Petro kuonyesha umati ule wa watu ufufuo wa Kristo ulithibitishwa na Agano la Kale. Waume pia walieleza jinsi walivyomwona Kristo baada ya kufufuka. Lakini mfano wa ajabu kuliko zote ulikuwa njia ile ambayo Roho Mtakatifu alikuwa akifanya ndani yao.

Ni jinsi gani Petro alianza mahubiri yake? Alianza kwa kumwita Kristo "Yesu wa Nazareti." Hili ndilo jina ambalo Wayahudi walitumia kuonyesha jinsi hawakumthamini Yesu. Ilikuwa njia yao ya kumdhihaki Yesu.

Bila shaka walishangaa kusikia mmojawapo wa wanafunzi wa Yesu akimwita "Yesu wa Nazareti." Lakini Petro alitaka wajue kwamba angewaambia habari za mtu yule yule ambaye wengi wao walikwisha kumdharau. Petro aliwakumbusha juu ya miujiza ambayo walimwona Yesu akifanya. Je! miujiza hii haikuthibitisha kwamba Yesu alitoka kwa Mungu?

Lakini Wayahudi walikuwa wamesisitiza kwamba Warumi kumsulibisha yule ambaye Mungu alikuwa amekwisha kuthibitisha kuwa ni Mwanawe. Petro aliwashtaki kwa kumwua Yesu. Wayahudi walikuwa na matumaini ya kwamba kuuawa kwa Yesu ndio ungekuwa mwisho wake. Lakini je! Mungu alifanya nini na Mwanawe huyu ambaye alikuwa amesulibiwa? Mungu alikuwa amemfufua katika wafu. Yesu alikuwa hai tena.

Wakati Petro alipowaambia watu wale habari za kuja kwa roho Mtakatifu, alikuwa akizungumza juu ya maandiko ya kitabu cha Yoeli cha Agano la Kale. Sasa aliwaambia mambo yaliyosemwa na mwandishi mwingine wa Agano la Kale. Aliwaambia mambo ambayo Daudi





# MASHAHIDI WENYE USHUJAA

MASOMO YA BIBLIA: Matendo 4:1-22

## KUJIANDAA KUFUNDISHA

Katika somo hili tunaona mwanzo wa mateso ambayo tutajifunza habari yao katika maandiko yaliyobaki ya kitabu cha Matendo ya Mitume. Mitume wale wawili (Petro na Yohana) waliwekwa gerezani jioni halafu kesho yake waliletwa mbele ya baraza ambapo walitishwa. Hatia yao ilikuwa ni kufundisha kwamba Yesu alikuwa amefufuka katika wafu. Wanafunzi, bila shaka, watavutiwa na ushujaa ambao Petro na Yohana walionyesha.

Kusudi la kufundisha somo hili ni kuonyesha kwamba Petro alikuwa shujaa katika uaminifu wake kwa Kristo, hata wakati alipodhihakiwa. Wasaidie vijana kuwa na uaminifu zaidi katika Kristo kwa kuelewa kwamba Yesu hutupa sisi pia nguvu ya kuwa mashujaa.

Soma Matendo 4:1-22 mara kadha mpaka ujue hadihti hiyo vizuri. Kwanza, ujifanye kuwa Petro. Kisha, ujifanye kuwa kiwete. Halafu, jaribu kufikiria njia ambayo watu wa baraza lile la Wayahudi walivyowaza mioyoni mwao. Jaribu kuwaongoza vijana kuzungumza jinsi wanavyoweza kuwa waaminifu kwa Kristo.

## MAMBO YA KUKAZA

1. Petro na Yohana walikamatwa na viongozi wa dini na kuletwa kuhukumiwa.
2. Kwa nguvu za Roho Mtakatifu, watu hao wawili walihubiri na kushuhudia kwa ushujaa ya kwamba Yesu alikuwa amefufuka katika wafu.
3. Baraza liliwaamuru Petro na Yohana wasiseme wala kufundisha habari za Yesu, lakini Petro aliwaambia ya kuwa angeendelea kushuhudia ukweli.

## KULIFUNDISHA SOMO

Jaribu kufikiria wakati maishani mwako ambapo unapata ugumu kuwa mwaminifu kwa Kristo. Je! ni wakati wa ibada kanisani? La. Lakini wakati mwingine tunapokaa pamoja na watu ambao hawamjui Yesu, tunakuwa na jaribu la kutaka kuficha ukweli kwamba sisi ni baadhi ya jamaa ya Mungu.

Katika Mathayo 10:32-33 tunasoma maneno haya, "Basi, kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni. Bali mtu ye yote atakayenikana mbele ya watu, nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni."

Kumkiri Kristo maana yake ni kuwa na nia ya kupokea uaminifu wetu kwake, pamoja na Wakristo wengine, bali ni katika mahali po pote tulipo. Ikiwa unahitaji ushujaa wa kumsimamia Yesu, tutafute jibu la swali hili: NAWEZAJE KUWA MWAMINIFU ZAIDI KWA KRISTO?



Mponywa alishika Petro na Yohana.

Soma sehemu ya kwanza ya mahubiri yenye nguvu ambayo Petro aliwahubiria Wayahudi. Katika kila mstari ulio kando ya sentensi zifuatazo hapo chini andika namba ya kifungu kinachoelezwa habari zake. (Matendo 3:12-16)

15 Mlimwua mkuu wa uzima, lakini Mungu amemfufua; na sisi tumemwona.

16 Kwa imani katika jina la Yesu, mtu huyu amepata nguvu na uzima.

13 Mungu amemtukuza Mwanawe Yesu, ambaye ninyi mlimsaliti na kumkana mbele ya Pilato.

12 Mbona mnatukazia macho sisi, kana kwamba tumemfanya huyu aende kwa nguvu zetu sisi?

14 Mlimkataa Yesu, Mtakatifu wa Mungu, mkataka mwuaji afunguliwe.

Kisha Petro aliwaambia watu wale ya kwamba hawakujua mambo waliyoyatenda walipomwua Yesu. Ni neno lipi katika Matendo 3:17 linaloonyesha jambo hili. KUTOKUJUA

Ni nani aliyekuwa ameandika tangu zamani kwamba Kristo angeteseka? **MANABII WOTE (kifungu cha 18)**

**Petro aliwaambia watu wale kufanya nini? TUBUNI na MREJEE.**

**KIFUNGU CHA KUKUMBUKA**

**"Mwimbieni Bwana, nchi yote; Tangazeni wokovu wake siku kwa siku." 1 Mambo ya Nyakati 16:23**

**Inatupasa kuwatia wanafunzi wetu moyo bila kuchoka kwa kumshuhudia Yesu. Tukitaka kuonyesha kila siku wokovu wake tunahitaji kuishi maisha ambayo Yesu anataka. Kwa vijana jambo hili mara kwa mara ni gumu sana kwao. Wewe, kama mwalimu na rafiki yao, una nafasi nzuri sana kuwasaidia wapate kuona umuhimu wa ushuhuda wao wa Bwana. Tukiwa kama Petro, pengine hatuna kitu cha kutoa isipokuwa habari njema ya wokovu, lakini ndicho kipawa kikuu kuliko zote!**

**WAKATI WA KUFUNGA**

**Je! wewe ni shahidi wa namna gani? Wewe ni kama Petro, na kumshuhudia Yesu Kristo kwa ushujaa? Au wewe hushiriki wokovu wako na wale ambao hawajakutana na Yesu? (Usingojee wanafunzi wajibu, bali wafikirie maswali hayo.)**

**Funga darasa kwa maombi ukimwomba Mungu kumsaidia kila mmoja kuwa na nia ya kushuhudia uwezo wa Yesu Kristo kila mara wanapopata nafasi.**



aliyasema. Aliwaonyesha jinsi Daudi alivyotabiri habari kuhusu kifo cha Kristo.

Lakini, ufufuo wa Yesu haukutabiriwa na Daudi peke yake. Ulionekana pia na mitume. Watu hawa wangethibitisha kwamba alikuwa amefufuka kwa sababu walikuwa wamemwona na kuzungumza naye baada ya yeye kufufuka katika wafu. Na sasa, kwa sababu Roho Mtakatifu alikuwa amekuja, ilikuwa thibitisho zaidi ya kwamba Kristo ambaye watu wale walimwua kama mhalifu, ndiye aliyekuwa hasa Mwana wa Mungu.

Je! umepata kujisikia kuwa na hatia? Hivyo ndivyo ilivyokuwa katika mioyo ya watu waliokuwa wakimsikiliza Petro. Tunasoma ya kwamba "wakachomwa mioyo yao." Wengi wao walitambua jinsi walivyokuwa waovu kwa kumtaka Pilato kumsulibisha Yesu.

Unawezaje kuondoa mawazo mabaya? Hilo ndilo jambo ambalo wengi kati ya wayahudi wale walitaka kujua, kwa hivyo walimwuliza Petro na mitume wengine, "Tutendeje ndugu zetu?" Walitaka kufanya kitu ambacho kingesahihisha makosa waliyokwisha kufanya. Walikuwa wametenda kosa kubwa. Walikuwa wameondoa uhai wa Mwana wa Mungu.

Petro aliwaambia kufanya mambo mawili. Kwanza, walipaswa kutubu; yaani, walipaswa kugeuza fikira zao juu ya Yesu wa Nazareti. Mbeleni walidai kwamba Yesu alikuwa mwongo na wakamkataa. Mungu alikuwa amewaonyesha kwa ufufuo ya kwamba Kristo ndiye aliyekuwa Mwokozi. Sasa Petro alikuwa akiwaambia wasikitike kwa ajili ya dhambi yao. Baada ya wao kutubu, wangebatizwa. Ubatizo ulikuwa ishara kwamba walikwisha kugeuza fikira zao za kumkataa Mungu na Mwokozi wao. Mungu aliahidi kwamba kama wangetubu na kubatizwa, wao pia wangepokea kipawa chake cha Roho Mtakatifu.

Wengi walifurahi kuamini ujumbe wa Mungu wa wokovu. Kabla ya siku ile ya Pentekoste kwisha, watu wapatao elfu tatu (3,000) waliamini! Yesu mwenyewe hakuwageuza umati mkubwa kama huu wa watu kwa wakati mmoja. Lakini alikuwa amewaambia mitume wake ya kwamba wangefanya kazi kubwa kuliko yake aliyofanya kwa sababu alikuwa akienda kwa baba yake. Roho Mtakatifu alikuwa sasa ameenea kila mahali.

**KAZI YA KUFANYA**

Petro alizungumza juu ya watu wawili ambao walikuwa wameandika katika Agano la Kale. Chora mstari kutoka kwa jina la kila mmoja hadi kwa maneno aliyoyaandika.

Mfalme Daudi Mungu atatoa Roho yake Mtakatifu kwa vijana na wazee, kwa wanaume na wanawake. Kila atakayeliita jina la Bwana ataokolewa.





Mungu atamfufua Mwanawe Mtakatifu. Siku moja Nabii Yoeli Mungu atanifufua mimi pia katika wafu.

Watu walichomwa mioyo yao waliposikia dhambi zao walizomtendea Yesu. Weka alama hii ( X ) katika picha ya moyo ulio mbele ya kila sentensi iliyo kweli.

 Petro aliwaambia kusahau kwamba walimwua Yesu.

 Petro aliwaambia watu kuamini kwamba Yesu ndiye Mwanawa Mungu na kubatizwa.

 Petro aliahidi kwamba wao pia wangepokea Roho Mtakatifu.

 Petro alisema, "Kila atakayeliita jina la Bwana ataokolewa."

Soma habari za Wakristo wa kwanza kutoka Matendo 2:44-47. Kata kila sentensi ambayo si kweli.

Walishiriki vitu vyote walivyokuwa navyo.

~~Waliwasaidia marafiki zao peke yake.~~

Walikwenda hekaluni siku zote.

~~Walilia kwa sababu watu wengine waliwadharau.~~

Walifurahi na kuendelea kumsifu Mungu.

Kila siku watu walikuwa wakiokolewa.

## KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

**"Na itakuwa kila atakayeliitia jina la Bwana ataokolewa." Matendo 2:21**

Ninyi pia mnaweza kuwa na furaha ya kuwa na Roho Mtakatifu mioyoni mwenu. Mungu anawaalika mliite jina la Bwana na kuokolewa katika dhambi zenu.

Someni tena kifungu chenu cha kukumbuka. Sasa choreni mviringo kwa majina ya watu watakaookolewa kama wakiliita jina la Bwana kuwaokoa.



WAZAZI



MWALIMU



Petro na Yohana hawakumpa kiwete yule msaada ule aliowaomba. Lakini walimpa msaada aliouhitaji zaidi mno. Kwa kufanya hivyo, walikuwa wajumbe waaminifu wa Yesu. Walimsikia mtu yule (kiwete) akitaka msaada, wakafanya kama Yesu angalifanya. Walimpa mtu yule upendo na kumponya kwa jina la Yesu Kristo, wakashiriki naye Habari Njema ya wokovu.

## KAZI YA KUFANYA

Siku moja, wakati wa alasiri; jambo fulani lilimpata mwombaji yule aliyeketi na kuomba katika mlango wa hekalu. Chora mstari kutoka kwa kila swali mpaka kwa jibu lake.

| | |
|---|---|
| Ni nani walio kuwa wakienda kusali? | Kiwete |
| Ni nani aliyekuwa karibu na mlango? | Petro na Yohana |
| Mtu yule aliketi katika mlango gani? | Pesa |
| Aliomba apewe nini? | Mzuri |

Kata shauri kwamba ni sababu zipi zinafaa mbele za Mungu. Weka alama hii ( X ) kwenye mstari ulio kando ya sababu unayofikiria kuwa inafaa.

Petro alimtaka Yesu kumponya kiwete kwa sababu:

____ Alimhurumia.

_X_ Alitaka kiwete yule kumjua Bwana.

Unamleta rafiki kwa Shule ya Biblia kwa sababu:

____ Mwalimu alimwambia kila mtu kumleta rafiki.

_X_ Unamtaka rafiki yako kumjua Yesu kama Mwokozi.

Soma Matendo 3:8-11. Kisha kamilisha sentensi zilizo chini ya kila picha.



Mponywa alitembea, akarukaruka akimsifu Mungu.



Watu walijaa na ajabu na mshangao

mnatukazia macho sisi, kana kwamba tumemfanya huyu aende kwa nguvu zetu sisi?" Matendo 3:12b.

Kisha Petro alianza kuwaambia habari za Yesu yule aliyewapa uwezo wa kutenda miujiza. Wayahudi walifikiri kwamba Wakristo walikuwa wakiabudu Mungu mpya. Lakini Petro aliwaeleza kwamba Yesu ndiye Mwana wa Mungu, Mungu yule ambaye wao na baba zao walimjua na kumwabudu. Ilikuwa kwa imani katika Yesu, Mwana wa Mungu, Petro na Yohana wakaweza kumponya kiwete yule.

Petro aliwakumbusha watu wale jinsi walivyomtesa Mwana wa Mungu. Walimkamata kama mfungwa. Pilato ambaye alikuwa liwali wa Kirumi alikuwa na tamaa ya kumfungua Yesu. Lakini Wayahudi wengine walikataa kumpokea Yesu kama Masihi, wakataka auawe.

"Lakini," Petro aliendelea, "Mungu amemfufua katika wafu na tu mashahidi wake. Yesu ndiye aliyemponya kiwete huyu."

Kama Petro angalikomea maneno hayo, watu wale wangalisikia vibaya sana baada ya kuwaambia ya kwamba walimwua Mwana wa Mungu. Lakini Petro alikuwa na habari njema pia. Kweli, walikuwa wamemsulibisha Mwana wa Mungu, lakini wao hata viongozi wao hawakujua watendalo. Mungu alikwisha kusema kwa manabii wote ya kwamba Mwanawe angeteseka. Kwa hivyo, kifo cha Kristo msalabani kilikuwa utimilizo wa sehemu ya mambo ambayo manabii wa Mungu walikwisha kusema na kuandika.

Walakini, watu wale waliokuwa wakimsikiliza Petro hawakuwa huru kutokana na hatia yao ati kwa sababu walikuwa hawajui Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Lakini wangeweza kupokea msamaha wa dhambi yao. Hiyo ndiyo iliyokuwa habari njema ambayo Petro aliwaambia watu hawa. Je! unaweza kukumbuka mambo ambayo Petro aliwaambia watu hawa kufanya ili dhambi yao ingeweza kuondolea?

Kitu cha kwanza ambacho Petro aliwaambia ni "Tubuni." Hili lilikuwa neno sawa na lile ambalo Petro alitumia siku ya Pentekoste akijibu swali la watu wale walilomwuliza wakisema, "Tutendeje, ndugu zetu?" Je! unakumbuka maana ya neno "tubuni?" Walipazwa kugeuza fikira zao juu ya Kristo na kutambua kwamba walikuwa wenye dhambi waliomhitaji Mwokozi kuwasamehe dhambi zao.

Petro waliwaambia ya kwamba, walipaswa kumpokea Kristo badala ya kumkataa, kuokolewa katika dhambi yao. Aliwaambia ya kwamba badala ya kuwa adui ya Mungu, walipaswa kuwa rafiki yake.

Wakati utakapojifunza somo lijalo, utaona ni idadi ngapi ya Wayahudi waliomsikia Petro siku ile akisema nao, wakaamini Habari Njema aliyowaambia na kumtegemea Kristo kuwa Mwokozi wao aliyewaokoa katika dhambi.





MARAFIKI

Petro alisema ujumbe ambao Roho Mtakatifu alimpa. Ni nani aliyechoma mioyo ya watu waliokuwa wakimsikiliza siku ile? Je! Petro au Roho Mtakatifu? Ndiyo ni Roho Mtakatifu. Kama watu wale wangalikataa ujumbe ule, wangalikuwa wanamkataa nani, Petro au Mungu?

Sisi ni sawa na watu wale. Hatusemi "La!" kwa mchungaji au mwalimu wa Shule ya Jumapili. Tunasema "La!" kwa Mungu ambaye anatupa wokovu.

**WAKATI WA KUFUNGA**

Ikiwa wewe ni Mkristo, labda utataka kuomba ya kwamba bwana atakutumia kama alivyotumia Petro. Pengine Bwana anakutaka kuwaambia wengine habari za wokovu wake.

Ikiwa wewe si Mkristo, usiseme "La!" kwa Mungu tena. Anataka upate wokovu unaohitaji.

Ongoza darasa lako kusema tena Kifungu cha Kukumbuka, kisha funga darasa kwa maombi.

# PETRO NA UWEZO WA MUNGU

**MASOMO YA BIBLIA: Matendo 3:1-19**

## KUJIANDAA KUFUNDISHA

Katika somo hili utaonyesha jinsi Roho Mtakatifu, akitumia Petro, alibadilisha ombi la mwombaji maskini kuwa nafasi ya kuonyesha upendo wa Kristo kwa mwombaji yule. Utaona jinsi Petro alivyoshiriki habari njema ya Kristo na watu wengi.

Wewe pia inakupasa kuwa macho kuyajibu maswali ya wanafunzi wako. Roho Mtakatifu anaweza kukusaidia kutumia maswali haya katika kushuhudia.

Ukitaka kufundisha bora ni lazima ujue mambo unayotaka kutimiza wawakati unapofundisha. Kusudi la somo hili ni kuonyesha kwamba Petro alitumia kila nafasi kumshuhudia Kristo: kuwasaidia wanafunzi kutambua ya kuwa wao pia wanapaswa kutafuta nafasi ya kushiriki habari za Kristo na wengine.

## MAMBO YA KUKAZA

1. Petro alimjibu kiwete wakati alipomwomba msaada.

2. Alimjibu kwa kumtimizia mahitaji yake yote.

3. Kiwete, aliyeponywa na mwenye furaha, alimsifu Mungu hadharani.

4. Watu walipokusanyika Petro alitumia nafasi hiyo kuwahubiria habari njema ya wokovu.

## KULIFUNDISHA SOMO

**Anza darasa kwa kuimba na kuomba. Waulize wanafunzi kutaja mambo mengine ambayo wangependa kuwekwa katika maombi.**

**(Sema:) Baada ya Siku ya Pentekoste, watu wengi walimwamini Yesu na kuwa wafuasi wake. Waamini hawa wapya walikutana kila siku kujifunza maandiko na kufurahia kula pamoja. Waliomba pamoja na kushiriki vitu vyao vyote.**

**Kila siku saa tisa za alasiri, Wayahudi walikwenda hekaluni kuomba. Hata siku moja alasiri, Petro na Yohana walikwenda hekaluni kusali. Walipitia mlango ulioitwa Mzuri. Wakasimamishwa na kiwete. Kiwete yule hakuweza kutembea tangu kuzaliwa kwake, na sasa alikuwa na umri uliozidi miaka arobaini.**

**Kila siku marafiki wake walimbeba na kumweka karibu na Mlango Mzuri wa hekalu ambapo aliwaomba pesa wale walioingia ndani kuabudu. Petro na Yohana walipopitia mlango ule, kiwete yule aliwaomba pesa.**

**Petro na Yohana walisimama kumtazama kiwete yule. Alikuwa hajiwezi na pengine alikuwa mchafu. Lakini alikuwa mwanadamu aliyeumbwa na mfano wa Mungu. Wanafunzi wale (Petro na Yohana) walitaka kumsaidia.**





Petro alimwambia, "Tutazame sisi."

Kiwete aliwaangalia na kusikiliza. Lazima awe alihuzunika sana wakati Petro alipomwambia, "Mimi sina fedha, wala dhahabu, lakini nilicho nacho ndicho nikupacho. Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama uende." (Matendo 3:6)

Kiwete yule alijaa tumaini mara moja. Labda alikuwa akifikiri, "Watu hawa hawawezi kunipa pesa, bali wananiambia nisimame niende. Sijapata kamwe kuondoka hata kidogo na kutembea hatua hata moja maishani mwangu. Wanasema kwamba yanipasa kufanya hivyo kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti. Nakumbuka jina hilo. Alisulibiwa, lakini nakumbuka nilisikia hadithi juu yake kabla ya kufa kwake, hadithi jinsi alivyowaponya viwete kama mimi."

Petro alishika mkono wa kiwete yule. Kiwete akaona kwamba anainuliwa. Nguvu ambayo alikuwa hajapata kuwa nayo ziliingia kwa nyayo na vifundo vya miguu yake. Kwanza, alikuwa sasa anasimama, kisha alianza kutembea. Ndugu, ilikuwa kweli ya kwamba aliweza kutembea!

Je! wewe ungefanya nini kama ungeweza kutembea kwa ghafla baada ya kuwa kiwete tangu kuzaliwa kwako? Nafikiri ungefanya kama kiwete yule alivyofanya. Alirukaruka. Alipokuwa akiingia hekaluni pamoja na Petro na Yohana, alipaza sauti na kumsifu Mungu kwa sababu alijua kwamba Mungu ndiye aliyempa Petro na Yohana uwezo waliomponya nao.

Kama mtu kijijini chenu ambaye amekuwa kiwete sikuzote angeweza kutembea kwa ghafula. Watu wa kijiji hicho chenu wangefanya nini? Wangekuja kuona ajabu hiyo. Vivyo hivyo, mle hekaluni, watu walikuja na kushangaa kwa yale yaliyotokea. Walipomwona kiwete yule, ambaye walikwisha kumwona mbeleni akiomba sadaka mlangoni mwa hekalu, walishangaa. Waliwaangalia Petro na Yohana katika Tao la Sulemani lililojengwa katika sehemu ya mbele ya hekalu. Na baada ya muda mfupi watu wengi walikusanyika kumwona kiwete yule aliyekuwa ameponywa na wale waliomponya.

Petro na Yohana walijua kwamba wao hawakustahili sifa. Ni nani aliyewapa uwezo wa kumponya kiwete yule? Ndiyo, Yesu Kristo.

Petro alianza kusema na watu wale. Aliwauliza, "Enyi Waisraeli, mbona mnastaajabia haya au mbona